# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Machi 24, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581625

www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US


UKURASA WA 2

**Watumishi** wadaiwa kutafuna mamilioni ya TASAF



UKURASA WA 5

**Wajanja** waibuka kutaka kujengewa nyumba Hanang

UKURASA WA 11

MAKALA MAISHA

**Mimi** na mume wangu ndoa iliyeyuka jumla



PICHICHI TURBAN-3

**VAZI 'KOTI LA MAMA SAMIA' LIMEMPAISHA**

UKURASA 13

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com



SAKATA MISHAHARA WABUNGE

# Mbowe, Bunge wazidi kuvutana

UKURASA 2



Foleni kubwa ya vyombo vya moto imetokana na maji kutuama kwenye barabara ya Nyerere Vingunguti, jijini Dar es Salaam iliyosababishwa na mvua kubwa za masika jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bilionea Sabodo afariki dunia

UKURASA 2

MAKALA MAALUM

## Wajane wasimulia magumu malezi ya watoto bila wenza

• **Watoa** somo kwa wenzao kuwalinda, kuwaombea waume zao... *Endelea Ukurasa wa 4*

**MICHEZO** WACHEZAJI YANGA WASAKA NGUVU 'GYM' UK.24

**KATUNI** UK.6

# Bilionea Sabodo afariki dunia Dar

**Na Beatrice Shayo**

MFANYABIASHARA maarufu, Mustafa Sabodo (82), amefariki dunia akiwa nyumbani kwake, Masaki, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mtoto wa marehemu, Dunstan, Sabodo alifariki dunia jana na kwamba anatarajiwa kuzikwa jana katika makaburi ya Upanga, Barabara ya Bibi Titi Mohamed karibu na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) majira ya saa 4:30 usiku.

"Mzee amefariki leo (jana) alfajiri akiwa nyumbani na taratibu za mazishi zinaendelea,"alisema Dunstan.

Sabodo alizaliwa mwaka 1942 mkoani Lindi na aliwahi kusema ametoka kwenye familia yenye utajiri wa imani na fedha.

Mwaka 2000, Sabodo alipatwa na ugonjwa wa kiharusi licha ya kuwa na changamoto hiyo aliendelea kufanya kile alichoweza kusaidia miradi ya kijamii.

Sabodo alifanya biashara katika nchi za Kenya, Ufaransa, India, Sudan na Zimbambwe na alikuwa akichangia miradi ya maendeleo ya huduma za jamii pamoja na uimarishaji wa demokrasia.

Enzi za uhai wake, aliwahi kuchangia fedha kwa nyakati tofauti kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ikiwa ni pamoja na kusaidia kampeni za uchaguzi za vyama hivyo .

Sabodo atakumbukwa kwa mchango wake ulioanzisha Mwalimu Nyerere Foundation National Lottery alipotoa msaada wa Sh. milioni 800.

Alihusika katika utoaji wa misaada mbalimbali ikiwamo kwenye kilimo, kujenga shule, hospitali, ujenzi wa visima 280 nchini kutoa msaada wa baiskeli na kusaidia wenye uhitaji.



Profesa Purity Gatobu kutoka Chuo Kikuu cha All Nations Christian Church International University kilichopo Texas Marekani (ANCCI) (kushoto), akirekebisha joho la Mkurugenzi wa Shule za St Mary's Dk. Rose Rwakatale (Katikati), ambaye alitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima (PhD) na chuo hicho jana Kibaha Mkoa wa Pwani. Kulia ni Angella Bondo, ambaye naye alitunukiwa shahada hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbowe, Bunge wavutana sakata la mishahara mipya ya wabunge

**Na Waandishi Wetu**

BUNGE na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wameibua mjadala mpya kuhusu wabunge kujiongezea mishahara kutoka Sh. milioni 13 hadi 18 kwa mwezi.

Wakati Mbowe akiibua suala hilo akiwa katika mkutano wa hadhara Babati mkoani Manyara, Bunge limekanusha madai hayo na kusema ni uzushi, hivyo yanapaswa kupuuzwa na Watanzania.

Alhamisi wiki hii, wakati akihutubia mkutano huo, Mbowe alisema mishahara ya wabunge kwa mwezi imeongezwa kwa kiwango hicho tangu mwaka jana.

Kutokana na madai hayo, Ofisi ya Bunge katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, ilisema kauli hiyo ni uzushi na upotoshaji kwa kuwa hakuna mbunge aliyeongezewa mshahara.

"Tunapenda kuujulisha umma kwamba taarifa hizo ni za uzushi na upotoshaji kwa kuwa hakuna mbunge aliyeongezewa mshahara kama alivyodai (Mbowe).

"Hivyo, tunapenda kuwashauri na kuwasihi wananchi kuzipuuza taarifa hizo ambazo lengo lake ni kuleta taharuki pamoja na kuwagombanisha wananchi na wawakilishi wao," ilisema taarifa ya Bunge.

Aidha, taarifa hiyo ilifafanunua kuwa nyongeza ya mshahara ni suala linalozingatia bajeti na hakuna utaratibu wa aina yoyote kama huo ambao umefanyika kwa ajili ya kuwaongezea waheshimiwa wabunge mishahara.

Akihutubia wananchi wa Babati, Mbowe alidai kuwa wabunge wamejiongezea mishahara hiyo kwa mwezi wakati wananchi wanataabika na upandaji wa bei za bidhaa na hali ngumu ya maisha.

"Mpaka tunatoka bungeni (2020), mimi na (Godbless) Lema tulikuwa wabunge tunajua tunalipwa mshahara wa Sh. milioni 13. "Hiyo ni bila ya posho ya siku ya kikao. Posho ya kikao kimoja kwa siku ilikuwa Sh. 220,000," alisema.

**MBOWE AJIBU**

Nipashe ilipomtafuta jana Mbowe ili kufafanua kauli yake na kilichotolewa na Bunge, alilitaka Bunge liseme fedha walizokuwa wanalipwa wabunge kabla ni kiasi gani na mwaka huu wanalipwa kiasi gani.

"Kama ni upotoshaji sasa wanalipwa kiasi gani? Posho ni kiasi gani? issue (suala) ni kwamba Bunge linatakiwa litoe takwimu kwamba jamani huyu mtu amepotosha. Sawa, inawezekana nimepewa taarifa za uwongo, sawa.

"Kinachotakiwa watoe takwimu walikuwa wanalipwa posho za kujikimu kiasi hiki, walikuwa wanalipwa za kikao kiasi hiki, za safari kiasi hiki na mwaka huu ni hizo hizo, au waseme ni shilingi ngapi.

"Waweke data (takwimu) hadharani kuliko kutoa 'statement' (taarifa) ambayo haina takwimu hata moja, wanatumia takwimu nilizozisema. Watoe za kwao ambazo ndizo halali ili kumaliza ubishi. Kwani shida iko wapi?"alihoji Mbowe.

# Watumishi wadaiwa kutafuna mamilioni TASAF

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya watumishi wa Halmashauri ya Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, wanadaiwa kuhujumu zaidi ya Sh. milioni 39 walizotakiwa kuwapatia wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Fedha hizo ni kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kutoka Kata 18 kwa kuwalipa wanufaika kipindi kimoja badala ya vipindi vitatu kama ulivyo utaratibu.

Watumishi hao wanadaiwa kutumia fursa ya uelewa mdogo wa wanufaika kwa kuwapa fedha za kipindi kimoja, hali iliyoibua malalamiko kwa baadhi yao kuambizana wamelipwa vipindi vyote vitatu.

Malalamiko hayo yaliibuliwa jana katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na wananchi wa kata ya Isaka kujadili shughuli za kimaendeleo pamoja na kero zao uliomshirikisha mkurugenzi, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mbunge wa Jimbo hilo, Iddi Kassimu, ambaye walimtaka kuingilia kati ili fedha hizo zirejeshwe kwa wanufaika.

Mkazi wa Segese, Mussa Unyango, alisema walikuwa na vipindi vitatu hajawalipwa fedha za TASAF ambazo husaidia kukuza mitaji yao kwa wale wenye biashara ndogo pamoja na kilimo kwa kununua pembejeo lakini baadhi wamelipwa fedha zote na wengine wamelipwa kipindi kimoja tu.

"Sisi tunaomba mbunge uliingilie kati suala hili ili tufahamu tatizo ni nini baadhi yetu walipwe vipindi vitatu na sisi tunatoka kata za pembezoni tulipwe kipindi kimoja. Kama TASAF wameanza kutubagua tujue," alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Mfilingi Abdallah, alikiri baadhi ya watumishi kula fedha hizo kwa kutumia njia ya uelewa mdogo wa wanufaika kujinufaisha na sasa wamewabana kuhakikisha fedha zinarejea.

Alisema kati ya Sh. milioni 39 zinazodaiwa kuliwa, tayari Sh. milioni 22 zimesharejeshwa na zilizobaki ni Sh. milioni 17.

Alisema fedha hizo ni miongoni mwa Sh. milioni 49 ambazo zilitokana na hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha uliopita na watumishi waliohusika katika ubadhirifu huo, wamesimamishwa kazi na taratibu zingine za kisheria na kiutumishi zinaendelea.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mibako Mabubu, alisema ili kuondoa malalamiko hayo walikubadiliana kupitia kamati ya fedha ambayo ilimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri,Hamisi Katimba, kutoa fedha zilizobaki kwenye mapato yao ya ndani na kuwalipa wanufaika, huku wakiendelea kuwashughulikia watumishi waliohusika.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alitoa siku saba kuhakikisha fedha hizo zinapatikana na kuwafikia walengwa wa TASAF ikiwa ni pamoja na kupata taarifa ya hatua zilizochukuliwa kwa wahusika waliokula fedha hizo kwa kuwa, wamefanya kosa kwa mujibu ya utumishi wa umma.

Mbunge Kassimu alisema hatakubali kuona wananchi wanapokonywa haki zao zinazotakiwa kupewa kisheria.

Alisema atahakikisha anakula sahani moja na wahusika hao na kuwataka wengine wenye tabia za namna hiyo kuacha mara moja, kwani fedha hizo zinatolewa kwa lengo la kumaliza umasikini na sio vinginevyo.

## TANGAZO


Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
Jiandae kwa
bashasha la kipekee.
Tunahesabia tu siku...
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com

MAKALA

# Wajane waibua magumu malezi watoto bila wenza

## -Wataka wenzao kuwalinda, kuwaombea waume zao wangali hai

Na Romana Mallya

JARIBU kufikiri kuhusu kauli hii ya Katibu wa Chama cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT), Sabrina Tenganamba (55) akitoa ujumbe mahsusi kwa wanawake walio kwenye ndoa kwa sasa.

Anatumiz msemo katika jamii, kitunze ingali hai, kikifa hautakiona tena, akiufafanua kuwa: "Utatamani kaburi lifunguke aamke mara ya pili walau aje akusumbue tu akupige vibao ili mradi watoto waendelee kumwona."

Ni rai yake akiwa na ushuhuda kwamba waliopoteza waume zao, wanapitia kipindi kigumu kulea watoto walioachiwa, kupata mahitaji na faraja wanapokabiliwa na sonona.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hii yaliyofanywa Alhamisi wiki hii jijini Dar es Salaam kuhusu mambo mbalimbali yanayosibu wajane, Sabrina aliwataka wanandoa kutambue kuwa wajane pia walipitia changamoto katika ndoa zao.

"Kuna wengine wanasema yamkini wajane mnaishi vizuri sana kuliko sisi ambao pengine wanaume wanatupasua vichwa, ninataka nikwambie, ninaapa mwanahabari na sisi waume zetu walikuwa wanatupasua kichwa, lakini ogopa sana atakapozikwa.

"Utatamani kaburi lifunguke aamke mara ya pili walau aje akusumbue tu akupige vibao ili mradi watoto waendelee kumwona. Tunachokiomba wanawake wenzetu si kwamba sababu tumebaki wanawake, muwalinde waume zenu na kuwaombea.

"Ujane ni afadhali upate Corona (UVIKO -19) au Ebola. Afadhali upate ugonjwa wowote mkali ukajua kwamba nitautibu vipi. Ujane hauna tiba, wengine wanasema utapata tiba kwa kuwa na mwanamume mwingine. Hapana. Mtoto anamhitaji baba. Hata yule mgumba anatamani labda mume wake wa ndoa angekuwapo, lakini hayupo. Niwaambie tu mtoto anahitaji baba asikwambie mtu.

"Wenye ndoa mtafute mbinu ya kuweza kutulia kwenye ndoa zenu. Ninamaanisha wanawake watulie kwa ajili ya watoto. Wanyamaze kimya. Wasiombee kwamba afadhali angekufa. Hapana. Kitunze kingali hai, kikifa hautakiona tena," alisema.

### MALEZI BILA WENZA

Sabrina anaainisha changamoto kubwa ambazo zinawakabili wanawake hao kuwa ni pamoja na kutengwa na ndugu, jamaa na marafiki kwa kukaa mbali na mjane endapo uchumi wake si mzuri.

"Kama una watoto wengi ndugu wanaogopa kuelemewa. Hii ni changamoto kubwa sana kwa wale ambao hawajaachwa vizuri. Ameachwa hana mali kwa lugha rahisi ni maskini.

"Hali za wajane ni uwiano wa 50/50. Wako walioachwa wakiwa tegemezi kwa waume zao lakini pia, wako ambao walinyang'anywa mali baada ya waume zao kufa na baadhi huogopa kwenda mahakamani. Lakini katika miaka hii mitatu iliyopita, mwamko wa wajane kudai haki umeongezeka," alisema.

Sabrina alisema kwa upande wa vijijini suala la mjane kupigania mahakamani haki ya mali alizoachiwa na mume bado ni tatizo. Alibainisha kuwa baadhi wakikabiliwa na uoga wakihofia kusimama na mashemeji katika mahakama.




Katibu wa Chama cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT), Sabrina Tenganamba

### KESI KUCHELEWA

Katibu huyo anataja changamoto nyingine ni wajane kukaa katika kesi miaka mingi bila kupata haki zao na mwisho wa siku kupoteza umiliki.

"Changamoto nyingine ni mjane anakuwa na kesi ya mirathi au ya madai. Pengine mume alikopa akaacha deni unakuta kesi inachukua miaka mingi na hapo anajikuta anatumia gharama za kwenda na kurudi mahakamani.

"Kuandika tu barua kwenda mahakamani inahitaji fedha, kutafuta wakili inahitaji fedha na hali hii wengine huishia kupata kiharusi au kupoteza mali kabisa hata kama ana haki.

"Hii changamoto ya kesi kukaa muda mrefu kama hana wakili imesababisha baadhi kukata tamaa. Kipo Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) wanatusaidia sana lakini unakuta kuna muda mjane mwenyewe anapokwenda kwa wakili anayemsaidia bure bado atalazimika kutumia fedha mfano nauli.

"Wengine wanakata tamaa kutokana na kesi kuchukua miaka mingi. Kuna mwanachama wetu ana kesi ina miaka 40 na yeye ana umri wa miaka 78 sasa. Kesi yake ni ya madai ya kudhulumiwa na rafiki wa mume wake maghorofa aliyoachiwa na mume wake.

"Mwingine ana kesi ambayo ina takriban miaka 20 mahakamani inahusu mkopo ambao mume wake alichukua benki. Kesi nyingine ambayo sasa ina miaka 15 ni ndugu wa mume wamekuwa wakikata rufani dhidi ya mjane kuhusu mali," alisema.

Pia alisema wajane walio wengi wanakabiliwa na changamoto ya mitaji hasa wenye umri wa miaka 55 kushuka chini na hiyo inatokana kukosa mali isiyo hamishika kutokana na kuachwa katika nyumba za kupangisha.

### WOSIA

Sabrina alisema baadhi ya wajane waliowapokea katika chama, waume zao kabla hawajafa waliacha wosia lakini ndugu walipojaribu kupora haki, walikwama kwa sababu serikali inasimamia uamuzi wao, wengi wanapata wanachostahili.

"Baadhi hudhani wosia ni kama mjane ameuandika mwenyewe ili kupata mali na wengine huuchukulia kama mjane amekusudia kuua mume ndiyo maana alilazimisha kuandikwa wosia. Tunasisitiza sana hasa wale ambao hawajapata majanga na wanaume ambao waliopo katika ndoa wafahamu kuwa, wosia si kifo," alikumbusha.

### SIMULIZI YAKE

Sabrina anafunguka kuhusu safari ya maisha yake kuwa: "Mimi mwenyewe nimeandika wosia kwa ajili ya watoto. Husaidia wale wanaobaki nyuma. Hatujui anatangulia baba au mama.

"Anaweza kutangulia yeyote. Wosia husaidia kutatua tatizo kwa jamii inayobaki hai hata ugomvi hautakuwapo wala mambo ya mahakama mara kwa mara hayatakuwapo. Hata sisi ndani ya chama tunasisitizana kuandika wosia," anaelimisha.

"Binafsi mume wangu ameniachiwa watoto watano na nina wajukuu wanane kwa sasa. Ninaishi eneo la Abiola huko Yombo, Temeke mkoani Dar es Salaam. Mume wangu hakuniachia mali. Nilizo nazo nimetafuta mwenyewe. Kifo chake kilitokana na ajali. Mimi na mume wangu tulinunua gari jipya tulipata ajali yeye alifariki dunia papo hapo.

"Ndugu wa mume walinitenga nikaonekana kisababishi cha kifo chake. Ndugu hawako karibu sana wa watoto wangu. Katika ajali ile iliyotokea mwaka 2004 niliumia mkono wa kulia ambao haufanyi kazi. Mume wangu akaniacha na watoto," anasimulia.

### TAWLA

Mkurugenzi Mtebndaji wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Wakili Tike Mwambipile, akifafanua kuhusu masuala ya kisheria na ucheleweshaji wa kesi uliolalamikiwa, alisema miaka ya hivi karibuni, mahakama ilitengeneza utaratibu kuhakikisha majalada hayachukui muda mrefu mahakamani.

"Kuchukua muda mrefu inategemea kama ilianzia mahakama za chini. Ila kuna jitihada ambazo zimewekwa na mahakama kuhakikisha kesi zinazoletwa zinasogea kwa haraka ili watu wapate haki zao.

"Zamani ndio kulikuwa na ucheleweshaji. Hii hatupingi lakini mfumo wa sasa wa kimahakama, unatambua na unategemea na kesi ina mambo gani ndani yake, lakini nyingi ndani ya miaka miwili zinatakiwa ziwe zimekamilika," alisema.

Wakili Mwambipile alisema katika masuala ya mirathi, ni changamoto ambayo huanzia kwenye sheria zilizoko zinazoangalia suala hilo. Alisema nchi ina sheria tatu za masuala ya mirathi ambazo ni sheria ya Kiislamu, sheria za kimila na sheria za kiserikali.

"Hiyo pia unaangalia maisha aliyoishi marehemu. Inachanganya ndiyo maana wanaharakati wengi na chama unachokisema (CCWWT) kwa umoja wetu tunataka sheria ifanyiwe marekebisho na kuwa na sheria moja ambayo inatizamwa kwa mapana.

"Ukitumia za sasa, mtu akienda kimila kuna watu watanyimwa haki zao wakati wanastahili kupata. Mapendekezo yetu ya sheria moja tunataka wale warithi halali wa marehemu wapate mali zao kihalali. Tumewahi kupeleka Sheria Pendekezwa serikalini kwamba, mfano wa sheria na Wizara ya Katiba na Sheria inayo huo mfano," alisema.

Kuhusu suala la wosia, alisisitiza ni muhimu kwa kuwa kulingana na changamoto ya sheria hizo mtu anapokuwa na wosia ndio utakaosaidia kupata haki kwa warithi halali kama ilivyoandikwa na hautaacha ugomvi.

ITAENDELEA KESHO...



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza na baadhi ya wajane mwaka 2022. **PICHA: MAKTABA**

# Serikali yanunua vifaa kudhibiti radi

**Na Faustine Feliciane**

KATIKA kukabiliana na changamoto kubwa kwa baadhi ya maeneo yanayoathirika na radi za mara kwa mara, serikali imenunua seti tano za vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani yaliyofanyika jijini Dodoma jana, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema vifaa hivyo vimefungwa katika mikoa ya Mara (Musoma), Mwanza, Kagera (Bukoba), Tabora na Kigoma (Kibondo).

"Hizi ni juhudi za serikali katika kukabiliana na matukio haya ambayo yamekuwa yakiathiri harakati za maendeleo katika maeneo hayo," alisema Mbarawa.

Pia alisema katika kukabiliana na janga la mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, serikali imeboresha huduma za hali ya hewa na uimarishaji wa mfumo wa utoaji tahadhari mapema (Early Warning Systems) nchini.

"Uboreshaji huu pia ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Ibara ya 59J ikiweka malengo ya kuimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa nchini.

Aidha, uboreshaji huu pia ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma za Hali ya Hewa ili kufika kwa jamii katika ngazi zote nchini kwa lengo hilo hilo la kukabiliana na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na kuhakikisha usalama wa chakula na afya pamoja na matumizi bora ya vyanzo vya maji," alisema Mbarawa.

Waziri Mbarawa alisema kwa kutambua kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa, vituo 15 vya kupima hali ya hewa vinavyojiendesha, vimenunuliwa na vitafungwa katika vituo vya utafiti na maendeleo ya kilimo ili kuchagiza utafiti kuhusiana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa sekta ya kilimo.

Pia Waziri Mbarawa aliipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa juhudi utendaji kazi wake ambao husaidia sekta mbalimbali nchini.

"Kama kaulimbiu ya mwaka huu ya maadhimisho ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani inavyoosema 'uwa Mstari wa Mbele Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi', nawapongeza TMA kwa kuwa mstari wa mbele kukabiliana na athari mbalimbali pamoja na kutoa taarifa za uhakika," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk Ladislaus Chang'a, alisema huduma za hali ya hewa zinazotolewa nchini zimeendelea kuwa bora zaidi katika historis ya tanzania kabla na baada ya Uhuru.

"Serikali ya Tanzania imefanya uwekezaji mkubwa katika ununuzi na uboreshaji wa miundo mbinu ya uangazi pamoja na wafanyakazi kujengewa uwezo," alisema Dk. Chang'a.

Alisema TMA imeendelea kuwa mstari wa mbele kutoa mchango katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi kwa kufanya utafiti na kuhamasisha matumizi ya sayansi kwa wataalamu wake na wataalamu wengine kwenye vyuo vikuu na taasisi za utafiti nchini na Afrika kwa ujumla.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (mwenye kofia), akimtwisha ndoo ya maji mkazi wa kijiji cha Gidagabara mkoani humo juzi baada kukabidhiwa mradi wa maji uliotekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania kwa kushirikiana na Wakala wa Usambazaji Maji vijijini (RUWASA), mradi huo umegharimu Sh Milioni 291.6. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajanja 500 waibuka kutaka kujengewa nyumba Hanang

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MFUMO wa Anwani za Makazi (NaPA) umebaini watu 500 walitumia udanganyifu kudai kuwa nyumba zao zilibomoka wakati wa janga la maporomoko ya matope katika eneo la Katesh, Hanang mkoani Manyara.

Wananchi hao walitumia udanganyifu huo ili serikali iwajengee nyumba mpya baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuahidi kwamba hakuna kitakachoizuia serikali kuwajenga nyumba za Sh. milioni 25 au 30 ili warudishwe kwenye maeneo waathirika wa maafa hayo.

Mratibu Msaidizi wa NaPA kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Arnold Mkude, alibainisha hayo jana wakati wa mafunzo kwa viongozi wa serikali Wilaya ya Singida yaliyofanyika katika ofisi ya mkuu wa wilaya.

Alisema baada ya kutokea janga hilo, kiliandaliwa kikosi kazi cha kitaifa kwa ajili ya kuisaidia serikali kubainisha nani amepoteza nyumba katika maeneo ya Gendabi na Katesh ambako wananchi wengi walikumbwa na maafa hayo.

Mkude alisema taarifa za awali zilionyesha kuwa kulikuwa na zaidi ya watu 600 ambao kila mmoja alikuwa anasema amepoteza nyumba yake kwa hiyo serikali izijenge kwa ajili ya kuwasaidia.

"Tulivyokwenda kule eneo janga lilipotokea baada ya kutumia mfumo wa anwani za makazi, tulibaini ni watu 100 tu ndio ambao nyumba zao zilibomoka kati ya 600 walioјitokeza.

"Kwa hiyo utaona namna ambavyo tumeisaidia serikali kuondoa udanganyifu kwa kuwa na taarifa za msingi kwenye ustawi wa taifa letu," alisema.

Katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, alisema umeanzishwa utaratibu wa utoaji wa barua ya utambulisho lengo ikiwa ni kuendana na kasi ya ukuaji wa uchumi wa kidigitali.

Alisema hatua iliyofikiwa ya utoaji wa barua ya utambulisho ni kwamba majaribio yameanza kufanyika kuanzia mwezi Machi hadi Mei, mwaka huu, na wadau katika suala hilo ni watendaji wa kata, mitaa, vijiji, watoa huduma na wananchi.

Mkude alisema lengo la majaribio hayo ni kubainisha upungufu na changamoto ili kuboresha kabla ya kuanza matumizi kwa nchi nzima. Alisema tangu operesheni ya anwani za makazi ianze, zimekusanywa taarifa milioni 12. 8 na zimewekwa nguzo za majina ya zaidi ya barabara 222,000 na vibao vya namba za nyumba zaidi ya milioni nne.

Mkude alisema shughuli kuu zinazofanyika katika utekelezaji wa mfumo wa NaPA ni kusajili majina ya barabara na kutoa namba za anwani za makazi, kukusanya na kuhuisha taarifa za anwani za makazi, kuweka miundombinu ya mfumo, kutoa elimu na kuwajengea uwezo kwa watekelezaji na watumiaji wa mfumo.

"Kuna manufaa makubwa ambayo yamepatikana tangu kuanza kwa mfumo huu. Kwa mfano kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) matumizi yalipoanza Aprili, 2023 katika kukusanya kodi ya majengo, kumesaidia kuongeza idadi ya maghorofa kutoka 4,164 hadi 32,000 na majengo ya kawaida kufikia 5,117,050 kutoka 2,988,546 yaliyokuwa yanatambulika kabla ya kuanza kwa mfumo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, akifunga mafunzo kuhusu anwani za makazi kwa watumishi wa serikali, taasisi binafsi na viongozi wa dini, aliwataka watumishi wa umma na watu binafsi kutumia NaPA katika kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema mfumo huo unarahisisha utoaji na ufikishaji wa huduma kwa urahisi na kuondoa usumbufu wa kutumia gharama kufika katika ofisi za serikali.

Gondwe ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema suala la mfumo huo linatakiwa kuchukuliwa kwa umuhimu kwa kuwa utafika wakati mtu anaweza kupata huduma serikalini au sehemu yoyote akiwa nyumbani kwa kuingia kwenye mtandao wa NaPA.

"Kila mfanyakazi wa serikali ambaye unajua kwamba unatoa huduma kwa wananchi ni muhimu sana na ni wajibu kupakua App ya NaPA ili kuweza kurahisisha katika ufuatilia na utoaji wa huduma kwa wananchi," alisema.

Gondwe alisema serikali imetengeneza mfumo wa NaPA ili kurahisisha huduma kwa wananchi hivyo unamhusu kila ambaye anafanya kazi serikali na asiye kwenye taasisi za serikali.

Alisema kwa watendaji wa kata mfumo huo utasaidia kupunguza siku za wananchi kupata huduma katika ofisi za kata.

Mtaalamu wa Mfumo wa Anwani ya Makazi kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Innocent Jacob, alisisitiza wananchi kuhakiki anwani zao na kutumia programu tumizi ya umma NaPA ili kuzijua kwa kuwa ni fursa katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Naye Mratibu wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mfumo wa Anwani ya Makazi kutoka wizara hiyo, Mhandisi Jampyoni Mbugi, alisema utumiaji wa mfumo huo utasaidia utoaji wa huduma na kuondoa matukio ya kiuhalifu kwa kuwa kila mtu atajulikana alipo.

Ofisa TEHAMA, George Leonard, alisema utaratibu wa utoaji wa barua za utambulisho utawarahisishia wananchi kupata huduma kwa njia ya mtandao.


**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE N. 4092/2024**

**In the matter of the Estate of the late of the late SARAH MOSES LYOKA of Mapinduzi within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY MAGDALENA MOSES LYOKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of 3, 2024
Date at Dodoma this **29th Day of February, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi wa kufuta leseni madini mwafaka, sheria iogezewe makali

**MADINI** ni moja ya sekta muhimu kwa maendeleo endelevu ya nchi pamoja na pato la taifa. Hiyo ni kutokana na Tanzania kujaliwa kuwa na aina mbalimbali za madini na vito ambavyo kama vitasimamiwa ipasavyo, vinaweza kuupaisha Uchumi wa nchi kwa kiwango kikubwa.

Mchango wa sekta hiyo kwa maendeleo ya Uchumi umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka, hivyo kuonyesha kuwa ni moja ya maeneo ambayo ni tegemeo katika kuifanya Tanzania kuendelea kupaa kimaendeleo na hata kuchangia ongezeko la fedha za kigeni kwa kuuza nje ya nchi.

Takwimu zinaonyesha kwamba mchango wa sekta hiyo kwa mwaka 2021 ulikuwa asilimia 7.2 ikilinganishwa na asilimia 4.4 ilivyokuwa mwaka 2017 likiwa ni ongezeko la asilimia 2.8. Pia katika robo ya tatu ya mwaka 2022/23 mchango wa sekta ya madini ulifikia asilimia 9.6.

Aidha, serikali katika kipindi hicho, kupitia sekta ya madini, ilikusanya Sh. bilioni 409.66 sawa na asilimia 85.43 ya lengo la mwaka la kukusanya Sh. bilioni 479.51 katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2022/2023. Hayo ni matokeo makubwa ambayo yanaonyesha kuwa sekta hiyo ni muhimu katika uchumi wa nchi.

Kutokana na maono ya serikali ya awamu ya tano katika sekta hiyo, mkazo mkubwa uliwekwa kwa kuwapo kwa masoko ya madini nchini pamoja na kuwapo kwa mitambo ya uchakataji ili kuyapa thamani badala ya kupeleka yakiwa ghafi kupitia makinikia ambayo yalikuwa hayabainishi kiasi halisi cha madini yaliyomo.

Aidha, kwa kutambua umuhimu wa madini, serikali iliweka jitihada za usimamizi madhubuti kuanzia utafiti, uchimbaji hadi mauzo kwa kuanzishwa kwa Tume ya Madini. Matokeo ya kuundwa kwa tume hiyo pamoja na wizara inayosimamia sekta hiyo yalianza kuonekana kwa kuongezeka mapato ya ukuaji wa sekta kwa ujumla.

Pamoja na jitihada hizo za serikali, imebainika kuwa wako baadhi ya watu sita wenye leseni za utafutaji wa madini, wakiwamo wanaomiliki ekari milioni 13.5 lakini hawazifanyii kazi. Pia imebainika kuwa katika leseni hizo kuna mtu mmoja ambaye pekee yake ana maombi 973 ya leseni ambazo zina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 23,118 lakini hafanyi kazi bali amezihisikilia tu.

Hatua hiyo imesababisha serikali, kupitia Waziri wa Madini, Athony Mavunde kuagiza Tume ya Madini kufuta leseni 2,648 za watu mbalimbali, wakiwamo waliojitwalia maeneo makubwa bila kuyafanyia kazi.


Waziri Mavunde, akitoa agizo hilo juzi, alisema kumekuwa na baadhi ya wamiliki wa leseni ambao wamekuwa hawazingatii utekelezaji wa majukumu yao ya umiliki kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura 123. Pia aliwaonya wanaoomba leseni kwa njia ya mtandao na kushindwa kuendeleza maeneo wanayopewa kuwa watachukuliwa hatua vinginevyo waache mara moja.

Kitendo hicho cha wamiliki wa leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini kushindwa kuzitumia, inarudisha nyuma nia njema ya serikali katika kutumia rasilimali za nchi kwa maendeleo ya wananchi katika sekta mbalimbali.

Ni wazi kwamba mapato yatokanayo na sekta hiyo, ni sehemu ya fedha zinazotumika katika maendeleo ya sekta mbalimbali kama vile afya, elimu, maji na miundombinu, hivyo kitendo cha watu kuhodhi maeneo bila kuendeleza shughuli za uchimbaji hakikubaliki. Uamuzi uliochukuliwa na serikali wa kufuta leseni hizo ni mwafaka kwa sababu una lengo la kuleta maendeleo na watu hao wanaokwamisha maendeleo kwa kuhodhi leseni na kukalia maeneo, hawana tofauti na wahujumu uchumi.

Licha ya uamuzi wa serikali kufuta leseni hizo, liko jambo la kujifunza na linapaswa kuwekwa katika Sheria ya Madini kwa kutoa muda maalumu kwa mwombaji kuanza kufanya kazi baada ya kupatiwa leseni. Kinyume cha hapo, mtu huyo anyang'anywe leseni ili wapewe wengine wenye nia na uwezo wa kutafuta na hatimaye kuchimba madini ili kuiletea nchi maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Miaka mitatu ya Rais Samia imerudisha siasa za ushindani

**LEO** ni siku ya sita tangu Rais Samia Suluhu Hassan atimize miaka mitatu madarakani, na sasa ameanza safari ya mwaka mwingine wa nne kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025.

Rais alikula kiapo kuongoza nchi Machi 19 mwaka 2021. Kabla ya hapo kulikuwa na malalamiko kutoka kwa vyama vya upinzani vikitamani kuwapo kwa uhuru wa vyama vya upinzani kufanya siasa za ushindani.

Malalamiko hayo yalitokana na zuio la mikutano ya hadhara ya vyama hivyo, lililowekwa na mtangulizi wake, hayati Dk. John Magufuli aliyeagiza madiwani na wabunge kufanya mikutano maeneo yao.

Zuio lingine lilikuwa ni la maandamano ya vyama kwamba viache serikali ifanye kazi, hatua ambayo ilisababisha malalamiko kutoka kwa wanasiasa na wadau wa siasa wakitaka vyama viwe huru kufanya siasa.

Katika kipindi cha miaka mitatu ambayo Rais Samia ameingia madarakani, amefanya mengi ya maendeleo, lakini bila kusahau siasa, kwa kuondoa zuio la mikutano na maandamano.

Rais amekuja kuboresha zaidi kile kilichowekwa na mtangulizi wake kwa kuweka wigo mpana wa kufanya siasa kwa kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa ambayo awali ilizuiwa.

Amefanya hivyo, kwa kuzingatia mazingira ya sasa kulingana na katiba na sheria kuwa haki kwa sheria za nchi vyama kufanya mikutano ya hadhara, hivyo hakuona sababu ya kuwapo kwa zuio hilo.

Matamanio yake ni kutaka wanasiasa wapambane kwa usawa kama njia ya kuimarisha demokrasia ili kuwaleta Watanzania pamoja ili wapinzani wakiwa na hoja zenye mashiko, anazichukua kuzifanyia kazi.

Kimsingi uhai wa vyama vya siasa ni pamoja na mikutano ya hadhara, ambayo ni jukwaa muhimu linalosaidia wanasiasa kutangaza sera za vyama vyao kwa wananchi ili waviunge mkono.

Hivyo, kwa mazingira hayo na umuhimu wake, ndio sababu Rais Samia akaondoa zuio hilo, ili kutoa uwanja sawa wa siasa kati ya CCM na vyama vya upinzani, lakini pia apate hoja zao na kuzifanyia kazi.

Maana yake ni kwamba, ameamua kutowafunga midomo ili wajimwage watoe ya moyoni badala ya kuendelea kulalamikia kutokuwapo kwa uwanja sawa kati yaa vyama hivyo na CCM.

Kupitia uamuzi huo wa Rais wa kuzingatia sheria na katiba ya nchi, hata CCM nayo inakuwa na nafasi ya kujirekebisha kama hoja za upinzani zitakuwa zinaigusa na hivyo kuendelea kuaminika mbele ya umma.

Ninaamini kuwa hiyo ni karata nzuri ambayo Rais ameicheza ya kupanua wigo na kurudisha upinzani wa kisiasa ili anufaike zaidi kwa hoja za wapinzani wasiwe na lingine la kupeleka kwa wananchi.

Uamuzi huo wa Rais Samia, unaonyesha kuwa anawachukulia wapinzani kama kioo chake cha kufanya marekebisho pale wanapotoa hoja zao ili yeye na serikali wazichukue na kuzifanyia kazi.

Lakini pamoja na hayo, ninadhani vyama vya upinzani, vingetumia nafasi hiyo vizuri hiyo kwa kutangaza sera za vyama vyao badala ya kashfa au matusi dhidi ya viongozi wa serikali.

Ikumbukwe kwamba, Rais amekuwa mtu ambaye anapenda kukosolewa, hasa kwa kutambua kuwa yeye si malaika, lakini pia ni vyema ukosoaji huo ukawa wa lugha ya kistaarabu.

Kwa kuwa ameruhusu kukosolewa, suala la kuzingatia mila na desturi za kitanzania katika ukosoaji ni la muhimu, hasa kwa kuzingatia kwamba hatua hiyo inasaidia kudumisha umoja wa kitaifa.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA

# Nabii hakubaliki nyumbani, Buriani Moses Mathew



Pascal Mayalla

**Pili, nitoe pole kwa TBC kumpoteza ripota wake mahiri. Pole hizi pia zinaandamana na pongezi kwa TBC kuubeba msiba huu. Pongezi hizi kwa TBC ni kutokana na Moses Mathew hakuwa mwajiriwa wa taasisi hii, lakini kwa kubeba jukumu, inastahili. Mtu unapokuwa ni correspondent tu, unafanya kazi kama kibarua, mwajiri anawajibika kukupa malipo ya jasho lako tu, lakini mengine yote, hayamhusu.**

KWA wiki tatu mfululizo, safu yangu imejikita kwenye Makala za Tanzia. Nilianza na Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi. Wiki iliyopita, ilikuwa ya mwanajamii mzalendo, Sanctus Mtsimbe, na leo ni mwanahabari Moses Mathew, mwandishi wa Habari wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Mwanza ambaye tumempumzisha jana kwenye nyumba yake ya milele.

Jina la Moses Mathew linaweza lisiwe maarufu kwa wengi kwa sababu mwanahabari huyu alikuwa ripota tu wa TBC Mwanza.

Kabla ya hapo alikuwa mwandishi wa Daily News kwa zaidi ya miaka 10 kisha akaandikia gazeti la East African, ndipo nikamwona TBC.

Tena ni baada ya kufariki dunia, ndipo nikajua kuwa kumbe hata TBC alikuwa mwandishi wa habari wa kujitegemea (correspondent) na si mwajiriwa rasmi. Alifariki dunia Jumatano wiki hii wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, jijini Mwanza.

Kwanza nitoe pole kwa familia yake kumpoteza mwanafamilia nguzo. Ni baba wa familia, mume, mtu aliyetegemewa na familia, ndugu, jamaa na marafiki. Poleni sana wanafamilia wa Moses Mathew.

Pili, nitoe pole kwa TBC kumpoteza ripota wake mahiri. Pole hizi pia zinaandamana na pongezi kwa TBC kuubeba msiba huu. Pongezi hizi kwa TBC ni kutokana na Moses Mathew hakuwa mwajiriwa wa taasisi hii, lakini kwa kubeba jukumu, inastahili.

Mtu unapokuwa ni correspondent tu, unafanya kazi kama kibarua, mwajiri anawajibika kukupa malipo ya jasho lako tu, lakini mengine yote, hayamhusu.

Lakini kwa TBC chini ya Dk. Ayub Rioba, hali ni tofauti. Kiukweli TBC imejitoa kikamilifu kuubeba msiba huu kikamilifu na huu si msiba wa kwanza, TBC imekuwa ikifanya hivyo hata huko nyuma. Huu ni upendo mkubwa kwa kuwajali sana watumishi wake. Tuwape maua Dk. Rioba na timu yake.

Nitoe pole kwa Klabu ya Wandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza na tasnia nzima ya habari kwa kumpoteza mwandishi mkongwe na mahiri wa habari.

Nilikutanishwa kwa mara ya kwanza na Moses Mathew na mwanahabari nguli Dotto Emmanuel Bulendu kupitia kipindi cha Jicho Letu Ndani ya Habari kinachorushwa hewani na kituo cha televisheni cha Star TV, hapo ndipo nilipomgundua Moses Mathew kuwa ni miongoni mwa waandishi wa habari wa vyombo vya utangazaji ambaye yuko wazi. Kwa maneno mengine si mtu wa kupindisha mambo. Nyeusi ataita nyeusi na nyeupe anaita nyeupe, kitu ambacho kilichangamsha sana Jicho Letu.

Baada ya Dotto Bulendu kupumzika, kipindi kiliendeshwa na Angalieni Mpendu, Moses Mathew akiwa miongini mwa washiriki maarufu na baada ya Angalieni Mpendu kustaafu, nilikabidhiwa kipindi hicho, Moses Mathew akiendelea kuwa mwalikwa maarufu.

Kwangu, ilinitokea bahati, nakabidhiwa kuendesha kipindi cha Jicho Letu. Siku ya kwanza nilikuwa na Moses Mathew na siku ya mwisho, nilipoaga rasmi kuendesha kipindi pale Star TV, niliaga kwa Aloyce Nyanda akiwa na Moses Mathew.

**NABII HAKUBALIKI KWAO**

Japo Moses Mathew kwa TBC alikuwa ripota tu ambako ni nyumbani, kwa jirani Star TV, alikuwa tegemeo sana. Kwa mujibu wa misingi na maadili ya uandishi wa habari, maoni ya mwandishi, si sehemu ya habari, hivyo Moses Mathew, hakutumia maoni yake TBC, bali aliyatumia Star TV, hivyo Moses Mathew aliyekuwa anaonekana Star TV, ni Moses Mathew maarufu zaidi kuliko yule Moses Mathew wa TBC kwa sababu, umaarufu wake Star TV yalikuwa maoni yake ambayo siku zote yanasimama, yaani hapindi, hakunji wala habembelezi!.

Kila baada ya kipindi, nilikuwa namshauri kwa nini asianzishe kipindi kama hicho TBC, yeye ni nguli wa rika langu, hivyo nikashauri, waandishi na watangazaji nguli wasifanye kazi za vijana. Suala la kuandika Habari tuwaachie vijana. Sisi manguli tuendeshe vipindi. Akaniambia pale si unapajua maana ulikuwapo, labda ninyi ndio mnisemee kwa wakuu wangu.

Moja ya sifa za ziada za waandishi wazuri wa habari, ni kitu kinachoitwa 'boldness'. Mwandishi unasimamia ukweli bila kujali kuwa ukweli huo utamfurahisha nani au utamchukiza nani. Kwenye ukweli, Mosses Mathew siku zote alisimama na ukweli na aliamini kwenye kweli na siku zote na alizungumza ukweli.

Siku za hivi karibuni kumezuka kada mpya ya vyombo vya habari na waandishi wa Habari. Hii ni kada ya vyombo vya habari vya kichawa na waandishi wa habari machawa!, Moses Mathew hakuwa miongoni mwao.

**BURIANI YA KUONANA**

Ndugu yetu Moses Mathew, japo sisi tulikupenda, Mungu amekupenda zaidi. Mwendo umeumaliza, imani umeilinda. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe. Buriani ya Kuonana, Moses Mathew.

**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kauli za majenerali Mabeyo, Mkunda si nyepesi



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

INGAWA Machi 19, mwaka huu, hakukuwa na shamrashamra za kumbukizi ya Rais wa Awamu ya Tano, Marehemu Dk. John Magufuli, lakini kauli aliyotoa Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali Venance Mabeyo, ilitosha kuwakumbusha Watanzania.

Jenerali Mabeyo akihojiwa na chombo cha Daily News Digital, alifichua nini kilijiri muda mfupi kabla na baada ya kifo cha kiongozi huyo, kuhusu kauli yake ya mwisho kwake lakini pia utaratibu wa kumpata na kumwapisha mrithi wake.

Kwa waliomwona Jenerali Mabeyo akisimulia kilichojiri akiwa mtulivu na makini katika kujieleza, ataamini kwa nini alistahili kuwa Mkuu wa Majeshi. Kwanza kwa uchaguzi wa maneno lakini hata nafasi aliyochukua wakati ule wa mpito.

Kauli yake ambayo imekuwa ikikaririwa na vyombo vya habari na baadhi ya watu wenye weledi wa kuchambua mambo, inaonesha kuwapo kwa sintofahamu katika kipindi kile cha baada ya kifo cha Rais Magufuli.

Watu walihoji sababu ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kutokuwa karibu na alikokuwa amelazwa bosi wake lakini Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na Katibu Mkuu Kiongozi, Bashiru Ally, kuwa wa kwanza kuarifiwa juu ya kifo hicho.

Itoshe tu kusema kama Jenerali Mabeyo asingesimama kidete kulinda Katiba ya nchi kama alivyoahidi kuilinda, pengine mambo yasingemalizika salama kama ilivyotokea kwa amani na utulivu. Hakika anastahili maua yake.

Pengine ndiyo sababu sijui ni kwa utani au vipi, watu kutoka Kanda ya Ziwa wamekuwa wakiaminika kwa kuwa na misimamo isiyotetereka, hivyo kusaidia mambo kwenda kama yalivyotokea chini ya Mkuu wa Majeshi huyo mstaafu.

Hivi najiuliza, kwa mfano Jenerali Mabeyo angekuwa na tamaa ya uongozi, nini kingemshinda au kumzuia wakati huo akiwa yeye na wadogo zake kiulinzi na kiusalama, kwenda tu pale TBC hatua chache kutoka hospitali ya Mzena na kutangaza kuwa sasa mimi ndiye!

Lakini kutokana na urahim wake, kutokana na ucha Mungu wake na hasa utiifu wake kwa Katiba, aliamua kusimamia utangazaji wa kifo cha Dk. Magufuli ukifanywa na Makamu wa Rais, lakini pia uapisho wa Rais mpya, Samia.

Hakika ili Tanzania iendelee kuwa ilivyo ikikua katika muktadha wa demokrasia, amani, utulivu, upendo na mshikamano, lazima twendelee kuteua wakuu wa majeshi kama alivyo Jenerali Mabeyo kwa mustakabali mwema wa taifa.

Muktadha huu unanifanya kufikiria kauli ya Mkuu wa Majeshi wa sasa, Jenerali Jacob Mkunda, kuhusu wageni na wakimbizi walioko nchini, ambao imefikia hatua mpaka nao wanateuliwa kuongoza ngazi ya kitaifa serikalini.

Jenerali Mkunda kama alivyo Jenerali Mabeyo, ni mmoja wa watu walioapa kuiheshimu, kuitii na kuilinda Katiba ya nchi, hivyo anapoona kuna masuala ya kiusalama yanachezewa, hana budi kuibuka na kusema.

Ndiyo sababu Januari 22, mwaka huu, alijitokeza mbele ya Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais Samia na kusema imegundulika kuwapo waomba hifadhi na wakimbizi walioajiriwa na kuteuliwa serikalini, jambo linalotishia usalama wa nchi.

Kwa nafasi yake, ni dhahiri ana vyombo vilivyofanya kazi ya kuangalia ni nini kipo na kinachoendelea, na hivyo kubaini kasoro na kuwa na uhakika wa anachokisema, kama alivyofanya Jenerali Mabeyo katika masuala la Magufuli.

Kwa uzito wa viongozi kama hawa, ni vema Serikali ikalifanyia kazi hili kwa uzito huohuo, hasa ikizingatiwa kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi wa serikali za mitaa na mwakani ni uchaguzi mkuu.

Endapo kauli ya Jenerali Mkunda itachukuliwa kama hadithi tu na kuachwa kama ilivyo, basi tujiandae kuchagua wageni kwa maana ya wasaka hifadhi na wakimbizi, kutuongoza katika mitaa yetu na hata katika taifa letu mwakani.

Si siri kuwa katika nafasi mbalimbali za uongozi mitaani, tunaishi na kuongozwa na wageni ambapo wamejivika utanzania, kwa sabbu moja au nyingine na kubwa ikiwa ni umri wa kuishi eneo husika.

Inabidi hili lifanyiwe kazi kwa kina, ili Tanzania ibaki kuwa ya Watanzania na uongozwe na Watanzania, na endapo mtu anataka uraia, basi afuate taratibu zilizopo za uraia na uhamiaji, badala ya kudandia maslahi ya wenye nchi yao.

Ni matumaini yetu Watanzania hasa tusio na nafasi za juu, kwamba maoni ya Jenerali Mkunda yatapewa uzito na kufanyiwa kazi katika kipindi hiki ambacho siasa zinatarajiwa kuchemka, husuan katika kutekekeza haki ya kidemokrasia.

Mungu Ibariki Tanzania!

# Waziri akemea ubaguzi sekta ya ardhi

**Na Munir Shemweta,**
RUANGWA

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amekemea baadhi ya watendaji wa sekta ya ardhi kuwahudumia wananchi kwa kuangalia hali zao, badala yake amewataka waache na watende haki kwa watu wote.

Pinda alisema hayo juzi wilayani hapa wakati wa kufunga mkutano wa wadau ngazi ya wilaya kujadili mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi nchini, mkutano uliofunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. "Katika kutoa huduma hizi tusiangalie hali ya mtu bali tuangalie haki ya mtu na huo ndio msingi wa wizara kwa kuwa hapa Ruangwa leo vinaitwa vijiji kesho ni mji, hivyo wanaweza kuja watendaji wengine wakaanza kusema michoro haikuzingatiwa kwa kuangalia hali ya mtu, hiyo haiwezekani," alisema.

Aliwaeleza watendaji hao kupitia mkutano wa wadau kuwa wanapopokea mwekezaji sehemu ambayo tayari ina mipango ya matumizi ya ardhi, taratibu zizingatiwe na kusisitiza pasiwe na suala la kuvamia vijiji vilivyowekewa mipango ya matumizi.

"Tukishafika katika kijiji kuna kamati ya ardhi. Hakuna mtu yoyote mwenye mamlaka ya kuuza ardhi ya kipande cha Kijiji. Lazima mkutano mkuu uitishwe kwa kushirikisha wale wote walioshiriki kupanga mpango wa matumizi ya ardhi," alisema.

Pinda pia alisema suala la ushirikishwaji wananchi kwenye kupanga mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji. Alisema ushirikishwaji wadau ni kipaumbele namba moja kwenye mradi wa uboreshaji miliki za ardhi na unaanzia ngazi ya kijiji hadi taifa kwa lengo la kuwafanya wananchi kuuelewa mradi ipasavyo.

Kwac wilaya ya Ruangwa, Pinda alisema ushirikishwaji umelenga kupata taarifa ya utekelezaji katika wilaya na baadaye wadau kutoa maoni yao. Katika mkutano huo wa siku moja, Waziri Mkuu ambaye alikuwa mgeni rasmi, alizindua Ripoti ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Vijiji katika wilaya ya Ruangwa na kutoa vyeti 18 vya ardhi ya vijiji.

Waziri Mkuu aliwaeleza washiriki wa mkutano huo kuwa nia ya serikali ya Tanzania ni kupima ardhi yote ili wananchi wakiwamo wanavijiji kuitumia kwa maendeleo ya kiuchumi.

Majaliwa aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri nchini kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kufanikisha mradi wa uboreshaji milki za ardhi nchini.

Mradi wa Uboreshaji Milki za Ardhi (LTIP) katika halmashauri ya wilaya ya Ruangwa, unalenga kuvifikia vijiji vyote kwa lengo la kuvihakikishia vinapata mafanikio.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikabidhi cheti cha kijiji kwa mmoja wa viongozi wa vjiji wakati wa mkutano wa wadau kuhusu utekelezaji Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi, uliofanyika Ruangwa mkoa wa Lindi, juzi. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# Watumiaji huduma za bima waongezeka

**Na Frank Monyo**

KAMISHNA wa Bima Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, amesema kupitia urahisi wa upatikanaji wa huduma za bima nchini, idadi ya watumiaji wa huduma hizo itaongezeka zaidi.

Amesema mwaka 2022 watumiaji wa bima walikuwa milioni 17.8 ambayo ni sawa na asilimia 28.9 ya Watanzania wote 61.7m.

Dk. Saqware alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati Kampuni ya Vodacom Tanzania kupitia huduma zake za VODABIMA, ikizindua kampeni kabambe ya Bima Kidijitali ambayo itanufaisha wagonjwa wa kulazwa na kutwa, vyombo vya moto (magari na pikipiki) na bima ya maisha kwa mtu mmoja mmoja na vikundi kwa gharama nafuu.

Alisema ubunifu wa kidijitali wa VodaBima utakuwa njia nafuu ya kupata huduma za bima ili kupunguza muda unaotumika kwa mtu kupata huduma hiyo na jambo hilo litawezekana kwa sababu mteja atatumia simu yake ya mkononi ili kuwafikia watoa huduma wa VodaBima.

Naye Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema baada ya kuzindua bima ya vyombo vya moto kwa kushirikiana na washirika 16 nchini, hivi karibuni walizindua Bima ya Afya ya mtu mmoja mmoja kwa kushirikiana na Assemble Insurance na Bima ya Maisha kwa mtu mmoja mmoja kupitia ushikirikiano na Sanlam.

Pia alisema walizindua bima ya maisha kwa vikundi kwa ushirikiano na Jubilee Insurance katika harakati za kampuni hiyo za kuongoza mapinduzi ya kuleta urahisi wa huduma katika sekta hii nchini kote.

"Tunafuraha kuzindua kampeni hii kabambe ya bima ambayo itajumuisha bima zetu zote kama vile 'AfyaPass' ambayo itawezesha wagonjwa wote wa kulazwa na kutwa kupata huduma katika hospitali mbalimbali nchini kote.

Huduma hii, ambayo inapatikana kupitia simu ya mkononi kupitia M-Pesa, inalenga kurahisisha upatikanaji na kuongeza wigo wa matumizi ya bima kwa kila mtumiaji. Tumefanikisha hili kutokana na unafuu wa gharama, ambapo gharama za mwaka ni Sh. 70,000 kwa kila mmoja. Pia unaweza kumwongeza mtu mwingine wakati wowote, sehemu yoyote kwa sababu kila kitu kinafanyika kupitia simu yako ya mkononi," alisema.

Aliongeza kuwa: "Pia tuna bima ya maisha ambayo inamhudumia mteja mmoja mmoja pamoja na bima ya maisha kwa vikundi."

"Uzinduzi huu unaendana na kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma za bima bila kujali hali yao ya kiuchumi. Kwa kutumia mtandao wetu mpana wa mawasiliano ya simu za mkononi, ambao unawafikia wateja zaidi ya milioni 20 nchi nzima. Tunaamini watu wengi watapata faida na kufikiwa kwa njia yenye ufanisi zaidi."

# Atunukiwa udaktari wa heshima kusaidia jamii

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Wazazi Mkoa wa Morogoro, Dk. Rose Rwakatale ametunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima na Chuo Kikuu cha All Nations Christian Church International (ANCCI) kilichoko Texas, Marekani kutokana na mchango wake kwenye jamii.

Hafla ya kutoa shahada hiyo kwa watu mbalimbali ilifanyika jana Kibaha kwa Mbonde mkoani Pwani na mwakilishi wa chuo hicho ambaye ni raia wa Kenya, Prof. Purity Gatobu.

Akizungumza baada ya kutunukiwa shahada hiyo, Dk. Rwakatale alisema kwa muda mrefu ametumia karama alizojaliwa na Mungu kusaidia makundi mbalimbali kwenye jamii wakiwamo wanawake, watoto na vijana kwa kuwapa nyenzo mbalimbali za kuwawezesha kuondokana na umaskini kama elimu ya ujasiriamali.

"Mimi pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Mkoa wa Morogoro, kwa hiyo wenye shida nimekuwa msaada kwao kwa njia mbalimbali na mimi ni mlezi wa Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni. Pale ninalea makundi mbalimbali kwenye jamii. Nashukuru sana kwa chuo hiki kunitambua kwa kazi zangu na imenipa moyo kwamba kumbe dunia inaona kazi ninayofanya," alisema. Dk. Rwakatale alisema shahada aliyotunukiwa imempa ari ya kuendelea kutumikia jamii kwa kutoa msaada mbalimbali kwenye jamii.

Angella Bondo, ambaye naye ametunukiwa shahada hiyo ya heshima, alisema kwa miaka 22 mfululizo amekuwa akitumikia jamii kwenye nyanja mbalimbali ikiwemo kutoa elimu ya ujasiriamali ambapo amefanikiwa kuwafikia watanzania wengi.

"Unaposaidia jamii unawagusa wanawake, watoto, vijana na hata wanaume. Kwa hiyo nashukuru kwamba chuo hiki kimeona kazi zangu na kuamua kunitunuku shahada ya udaktari wa heshima na naahidi kwamba hii itakuwa chachu ya mimi kuendelea kuitumikia jamii," alisema Bondo.

Pia alisema amekuwa akitoa huduma kwenye makanisa mbalimbali likiwemo la Mlima wa Moto Mikocheni kupitia vipindi vya redio na kwamba amepata tuzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kutokana na kazi zake ikiwemo ya kuwajengea uwezo wanawake ya kujiamini.

"Nimekuwa natumia muda wangu mwingi kuzungumza na kuwapa moyo wajane kwamba wanaweza kufanya mambo makubwa pamoja na hali wanayokabiliana nayo. Kwa hiyo nawahamasisha wasijisikie wanyonge wasimame na wafanye mambo makubwa na wengi wanaelewa somo na maisha yanasonga mbele bila wasiwasi," alisema.

# MAISHA

MACHI 24, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

PICHICHI TURBAN-3

## Vazi 'Koti la mama Samia' limempaisha



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Chukua tahadhari kuepusha majanga ya moto kwenye nyumba



Ukurasa 12

HARUSI




# Ondoa sugu kwapani

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | ■ | T | A | I | F | A |
| S | ■ | ■ | ■ | M | ■ | N |
| H | ■ | F | A | A | ■ | D |
| I | B | A | ■ | R | A | I |
| N | ■ | N | O | A | ■ | K |
| D | ■ | Y | ■ | ■ | ■ | I |
| I | D | A | K | E | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

DUA, NIA, WAO, RAI, IBARA, SHINA, DONDA, IMARA, UDIWANI, ANZISHA


## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na ragiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mimi na mume wangu ndoa iliyeyuka jumla!

***KARIBU** msomaji wangu tuendelee kudadavua vituko ndani ya ndoa zetu. Kila ndoa unayoiona ina changamoto zake. Na kila tikisiko kwenye ndoa lina chimbuko au chanzo chake. Hakuna kinachotokea kwa bahati mbaya.*

**"Mume pamoja na kuwa tulifunga ndoa nzuri, nilimfumania ndipo tukaachana moja kwa moja. Hatukwenda mahakamani wala kanisani kuvunja ndoa na mchezo ukaishia hapo.**

Maisha ya ndoa ni safari ndefu. Kuna wakati mtafurahi na kuna nyakati zitawalazimu kulia. Kuna wakati mtapishana katika uamuzi na wakati mwingine maisha ya uchumi wenu yanaweza kushuka uu kugongana mawazo au mmoja wenu aweza kuugua. Hapo ndipo upendo wa kujitoa unatakiwa kudhihirika kwa kila mmoja wenu.

Katika nyakati tunazoishi, yamekuwapo matatizo makubwa sana ya ndoa. Ndoa nyingi sana ziko katika hatua ya kufa au zilishakufa kabisa au wana ndoa wameshafungasha virago na ndoa zao kuzitupilia mbali kabisa.

Wanaume na wanawake wengi sana leo wanajitahidi kutafuta mbinu mbadala za kujiridhisha wao wenyewe kwa kuwa wameshindwa kabisa katika ndoa zao! Hebu sikia kilio cha mama huyu kwa yale aliyopitia kwenye ndoa yake aliyoipenda lakini akaitosa baada ya mambo kumfikia shingoni.

Anasema hivi kupitia ujumbe kwenye WhatsApp yangu: "Mume pamoja na kuwa tulifunga ndoa nzuri, nilimfumania ndipo tukaachana moja kwa moja. Hatukwenda mahakamani wala kanisani kuvunja ndoa na mchezo ukaishia hapo.

Lakini kabla ya kuachana nilitengana naye, nami kwenda kupanga chumba. Hili ni tatizo linalowapata kinamama wengi sana lakini matukio mengine yanaamuliwa kimya kimya." Huyu mama ni mkazi wa Ngaramtoni ambaye nilimkuta kwa rafiki yangu hivi majuzi.

Kaka mmoja naye baada ya kusoma makala ya wiki iliyopita, akanitafuta kunimegea kisa cha dada yake ambaye alinasa meseji za simu ndani ya simu ya mumewe na alipomwuliza,a mume huyo akawa anakana.

Katika hali iliyoonyesha ni kweli alikuwa akidhulumu ndoa yao baada ya kumshtukia, sasa akawa analalia simu chini ya mto ili mkewe asizipate na kuzichunguza.

Kwa maelezo yake anasema: "Dadangu ni mjasiriamali, ana duka lake la nguo Kariakoo. Mumewe ni injinia kampuni ya ujenzi. Ni wanandoa na tayari wana mtoto mmoja. Kabla ya ndoa, wawili hawa walipendana sana. Lakini matatizo yalianza mara tu baada ya mtoto kuzaliwa ambapo mume alianza vitimbwi.

"Mara aanze kurudi saa nane usiku, mara saa tisa na wakati mwingine alfajiri. Akiulizwa na mkewe hajibu. Siku moja akarejea akiwa amelewa sana, hivyo akajisahau mkewe akawahi simu mojawapo. Alipoipekua akagundua meseji kibao za mahaba. Akaamua kunakili namba za simu kisha kesho yake akaipiga namba ile kumwuliza kuhusu meseji zile.

"Mwanamke mwenye namba ile alipopigiwa akajibu kwa jeuri, matambo na matusi juu. Akasema kwani ndoa ni kitu gani. Ilibidi dada yangu amwulize mumewe kuhusu mwanamke huyo wa nje lakini akawa mkali na kukataa kwamba si kweli.

"Akadai ni mfanyakazi mwenzake na pia bosi wake, hivyo asimvunjie heshima. Na mkewe akamwambia kama ni bosi wako lazima niende kumwuliza lakini baada ya hapo mchezo ule ukajirudia.

"Yule bwana kuona mambo ni hadharani akawa mpole kwa takriban siku nne hivi baada ya kuona dadangu kachachamaa. Hata hivyo, alipoona mkewe ameshamshtukia akabadili simu akanunua zile za slid (kutelezesha vidole) ambazo dadangu hajui kuzitumia."

Swali ni je, kubadilisha simu ili mwenzio asijue yanayoendelea chini ya pazia ni ufumbuzi wa tatizo au unalizidisha? Ukweli ni kwamba tunahitaji sana msaada wa ki-ungu. Hali hii imekuwa ikisononesha sana.

Eneo hili la ndoa si la kupuuzia kabisa. Lazima tukae chini na kuanza kuchimbua jambo hili linalowatesa watu wengi. Pale tu tutakapogundua chanzo cha matatizo ya ndoa, nina hakika tutapata msaada kutoka kwa Mungu mwenyewe utakaobadilisha maisha yetu ya ndoa.

Katika eneo hili tunahitaji hekima ya Mungu, maana hekima ya binadamu haiwezi kutatua matatizo haya. Suluhu ya matatizo ya ndoa huanza pale tu mtu anapomruhusu Mungu kuingilia kati tatizo hili la ndoa. Hakuna tatizo la ndoa linaloweza kumshinda Mungu!

Huenda umeteseka kwenye ndoa yako kwa muda mrefu, huenda umeshakata tamaa kuhusu ndoa yako na labda umeapa hutakaa ujihusishe na mambo yoyote yanayohusu ndoa. Usiogope, Mungu anakwenda kjubadilisha ndoa yako!

***Je, una maoni, ushauri au kisa cha kimaisha? Ujumbe 0715268581. Namba ipo kwenye WhatsAPP.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Kuna jambo gumu linalonipa uchungu moyoni

HOJA ya Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, kuja na mbinu mpya za kuzuia upigaji kanisani, imenikosha na inanitia moyo.

Askofu Dk. Shoo ana jicho la tatu lisilo la kawaida. Jicho hilo ukilifungua utaona vitu vingi ambavyo wenzio hawaoni.

Jicho hilo likifunguka huwa halizibwi na kitu chochote, hata iwe kiza kinene mbele yako, utaona kama mtu aliyekuwa juani mchana. Ni jicho linalokupeleka kwenye maisha ya watu, utawajua watu majina na maisha yao; hata kama hawajakwambia.

Kauli ya Askofu Dk. Shoo kuhusu matumizi ya fedha mbichi kanisani, inatoa tafakuri ya kina kuhusu aina hiyo mpya ya uipigaji.

Amesema maneno yanayopasua ngoma za masikio yetu. Uwazi katika jambo kama hili, ni darasa tosha ambalo kila mmoja wetu anapaswa kujifunza.

Hakuna ubishi kwamba kwa kauli yake anaona kuna mwanya mkubwa wa upotevu wa fedha ndiyo maana anataka jicho kali zaidi liwekwe kungalia fedha mbichi zinazotumika bila kupelekwa benki.

Kwa jicho lake katika matumizi ya pesa mbichi, uko ulazima kama kiongozi mwenywe maono, kuhakikisha malipo yote yanayofanywa na sharika zote, yanapelekwa benki siku hiyo hiyo.

Ili kuepuka matumizi ya pesa mbichi kanisani, iwake, inyeshe, mapato yote yasibakie mikononi mwa wachache, hasa Wachungaji ili kuepusha matumizi ya pesa mbichi.

Iko haja ya kufuatilia na kuhakiki hati zote za malipo, zinakuwa viambatisho wakati wote, na isiwe tu mpaka wakati wa ukaguzi.

Kuwapo na vitabu vya kumbukumbu vinavyoonyesha kiasi cha fedha zinazopatikana kupitia vyanzo vyake mbalimbali, ikiwamo sadaka.

Mwanzoni mwa wiki hii, katika kikao chake na zaidi ya Wachungaji 300 wa Dayosisi hiyo, Dk. Shoo alieleza kile asichokubaliana nacho na akitaka kuepukwa huku akionya fedha za sharika zisitumike ndivyo sivyo, huku akihadharisha Wachungaji wasikubali kuruhusu matumizi ya pesa mbichi ambazo hazijapita kwenye vitabu.

Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, inaundwa na majimbo matano ya Kilimanjaro Mashariki, Kilimanjaro Kati, Hai, Siha na Karatu.

Askofu Dk. Shoo, ambaye amekuwa Mkuu wa Kanisa la KKKT kwa miaka minane, alikemea matumizi ya fedha mbichi kanisani wakati wa kikao kazi kilicholenga pamoja na mambo mengine, kuwakumbusha Wachungaji kuwa waadilifu katika masuala ya fedha, kazi na mienendo ya maisha.

Katika nasaha zake, Dk. Shoo alionya akisema kuna taarifa za fedha za Usharika kutumika ovyo, akibainisha wako baadhi ya Wachungaji wanatumia nafasi zao kushawishi watu wasiokuwa waadilifu na wasiojua wajibu wao katika Baraza la Usharika.

"Unakuta Mchungaji anasema, hebu nipe 100,000 hapo, pesa ambayo ni mbichi haijapita kwenye vitabu. Unapofanya hivyo, ni kukosa uaminifu na unafundisha wewe wale wengine. Hii haina baraka, taratibu za utunzaji fedha zifuatwe," alinukuliwa akiyasema hayo.

Aidha, Askofu Dk. Shoo aliwasihi Wachungaji hao kuendelea kutunza maadili ya utumishi.

"Ndugu zangu Wachungaji, tumeitiwa huduma hii takatifu kwa neema ya Mungu. Ninawakumbusha na kuwasihi sana, tutunze maadili ya utumishi na haya yanaanzia na wewe mwenyewe unavyoonekana.

How you behave (mwonekano wako ulivyo), usionekane kama Mchungaji wa kijiweni au mtu wa kijiweni, tafadhali! utumishi huu una heshima yake, maneno yako unayozungumza yatofautiane na maneno ya kijiweni; lakini tutunze maadili ya wito wetu," alisisitiza.

Kwenye hotuba yake, Askofu Dk. Shoo, aliwataka Wachungaji kuwa waadilifu katika masuala ya fedha na kuweka kumbukumbu za fedha kwa uadilifu na kufuata taratibu.

Uchungu ni hisia abebazo mtu baada ya kufikwa na jambo au maudhi fulani. Ni mwitikio wa kihisia uliosababishwa na tukio lililo mkosesha mtu amani moyoni.

Labda hujanielewa. Uchungu ni ishara ya awali kwamba kuna jambo lililosababisha uchungu moyoni, ambao imeshindikana kuachiria.

Katika Kitabu cha Isaya 38:15 imeandikwa. Niseme nini? Yeye amenena nami, na yeye mwenyewe ametenda hayo; Nitakwenda pole pole miaka yangu yote, kwa sababu ya uchungu wa nafsi yangu.

***• Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com na Simu ya mkononi: +255 715 545 490***

# HARUSI



Ilikuwa siku ya kipekee baada ya Faraji Mgeni 'Kipunje' alipofunga ndoa na Pendo Juma Kassim Februari 23, mwaka huu na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika nyumbani kwao Tegeta Bwawani mkoani Dar es Salaam.





# MITINDO

## PICHICHI TURBAN-3

# Vazi 'Koti la mama Samia' limempaisha











UMAARUFU wa mavazi ya Stara umeongezeka nchini na hata duniani kote, hivyo kuwafanya wabunifu kama Pichichi kufikiria nje ya boksi.

Hapa nchini umaarufu wa vazi hili umetokana na harakati nyingi yakiwemo majukwaa kama Stara Fashion Week, ambalo hufanyika kila mwaka .

Katika wabunifu wanaomuangalia kwa jicho la karibu, Said Ndee maarufu Pichichi Turban ambaye amebuni vazi la 'Juba la Ramadhan'

Katika sehemu ya tatu ya simulizi yake amatueleza jinsi vazi alilovaa Rais Samia Suluhu Hassan katika filamu ya 'Royal Tour' lilivyompatia umaarufu.

Ndee anasema mwaka 2021 alipata fremu maeneo ya Kariakoo karibu na Hoteli ya Wanyama na hapo aliamua kununua cherehani mbili, mmoja aliweka cherehani kwa ajili ya kushona na upande wa pili akaigeuza eneo la kuuzia kofia zake.

Saidi anasema duka hilo likawa ndiyo sehemu yake na wateja wake wote akawa anawaonesha, hata wafanyabiashara wadogo wadogo wakawa wanamfuata na siyo tena kuwapelekea mizigo.

Anasema tayari akili yake ikazama ni jinsi gani anaweza kutengeneza fedha zaidi, aliamini biashara ya kofia inaenda ipo siku itabadilika na huenda soko likapotea kabisa.

Anaongeza kuwa akafikiria kubuni vazi ambalo litaendana na kofia hizo, kwa kuwa hata wateja wake nao walipokuwa wakiagiza kofia kupitia mtandaoni walikuwa wakiuliza na mavazi watayapata wapi.

Saidi anasema kama ilivyokuwa kwa kofia aliweza kupambana na kubuni vazi lake la kwanza, ambalo aliliita jina la 'hijabu ya kisasa' ambalo aliliingiza sokoni mwaka 2021 na lilifanya vizuri zaidi.

Baada ya hapo akaanza kutengeneza mavazi mbalimbali na alijifunza kupitia uvaaji wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Rais alikuwa kama kioo kwangu, nikapata mawazo mengi na kujua naweza kubuni vazi gani la stara na heshima kupitia mavazi yake," anasema.

Kwa mara ya kwanza wakati anaingia madarakani, Ndee anasema aliweza kubuni vazi lililoitwa Koti la Samia, ambalo lilitokana na nguo zake za kitenge na koti na lilifanya vizuri sana.


Koti la mama Samia lilikwenda mbali zaidi na watu wakawa wanauza hadi katika nchi za jirani, ikiwemo Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na nchi zingine za jirani, ambapo vazi hilo lilipokelewa vizuri.

Saidi anasema kupitia vazi alilovaa Rais Samia katika filamu ya Royal Tour aliweza kubuni na kutengeneza vazi la Royal Tour ambalo lilikuwa ni viatu, kombati na kofia.

"Vazi la Mama Samia Tour lilishinda tuzo mbalimbali, ikiwemo hapa nchini na nchini Zambia... hili vazi lilikuwa maalumu kwa ajili ya kutangaza utalii wa ndani, na katika kila onesho watu wengi walikuwa wakiniuliza kwa nini niliiita jina hilo ndipo nilipokuwa napata nafasi ya kuitangaza nchi yangu kwa kuelezea," anasema.

Anasema akaanza kutengeneza mavazi kulingana na wakati na kuwa alitengeneza mavazi mbalimbali kama mavazi ya Corona alililotengeneza kipindi cha Covid-19 imepamba moto na kufunga vitakasa mikono, lakini alitengeneza kofia za Fly Over na mavazi mengine ambapo yalimpa jina ndani na nje ya nchi ikiwemo vazi la Mayotte lililopata jina la kisiwa cha Mayotte kilichopo Bahari ya Hindi kati ya nchi ya Comoro na Msumbiji.

UREMBO





# Ondoa sugu kwapani

SEHEMU ya ndani ya paja na kwapa kuna wakati inakuwa na rangi nyeusi inayosababishwa na msuguano wa ngozi.

Hili sio tatizo kubwa kama utakuwa makini katika kujitunza, na leo nimekuletea njia za asili za kuondoa weusi huo bila kutumia madawa makali.

### MAFUTA YA NAZI NA NDIMU

Mafuta ya nazi yanatumika kulainisha ngozi na pia huondoa weusi ukichanganya na ndimu.

Chukua vijiko vitatu vya mafuta ya nazi changanya na ndimu nusu, paka sehemu yenye weusi katika mapaja huku ukisugua kama unafanya masaji kwa dakika 15.

Kisha osha na maji ya uvuguvugu na kausha kwa kitambaa kilaini na kisafi.

### SUKARI, ASALI NA NDIMU

Mchanganyiko huu pia unaweza ukaondoa weusi katika mapaja na makwapa.

Changanya kijiko kimoja cha asali, ndimu nusu na kijiko kimoja cha sukari.

Paka sehemu yenye weusi na sugua kawaida hadi sukari ipotee.

Acha ikae kama dakika 10 kisha osha na maji ya uvuguvugu.

### GANDA LA CHUNGWA NA ASALI

Kama mnavyojua machungwa yana vitamin C na hivyo ukichukua ganda la chungwa pamoja na asali, mchanganyiko wake pia unaondoa weusi.

Chukua ganda la chungwa na kijiko kimoja cha asali. Kamua hilo ganda maji yake yaingie kwenye asali. Kausha na kusaga hilo ganda kisha poda yake ichanganye na asali.

Paka mchanganyiko huo katika sehemu yenye weusi, kaa kwa muda wa dakika 15

Osha na maji ya kawaida hadi kugandaganda kupotee.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya stafeli na tende



TENDE ni miongoni mwa matunda yaliyothibitishwa na wataalamu wa afya kuwa na faida lukuki mwilini mwa binadamu hasa pale linapotumiwa ipasavyo.

Licha ya baadhi ya watu kutumia tunda hilo kama chakula kamili, kifungua kinywa au kutengeneza sharubati yake, limekuwa pia likitumika katika utengenezaji wa juisi (sharubati) za matunda mengine ikiwemo stafeli.

### Jinsi ya kutengeneza

Maandalizi ya juisi ya stafeli na tende yanaanzia kwa kuosha stafeli na kuchambua mbegu zote zilizopo katika tunda hilo.

Katika hatua hii umakini unahitajika kwa sababu stafeli lina mbegu nyingi zilizojificha ambazo zisipotolewa zinaweza kuharibu blenda wakati wa kusaga.

Kisha maliza kuchambua mbegu kwenye stafeli, rudia zoezi hilo kwenye tende halafu uziloweke kwa nusu saa au zaidi kabla ya kuanza kusaga.

Baada ya kumaliza maandalizi andaa blenda kisha umimine stafeli ulilochambua mbegu, tende na kiasi cha maji.

Hapa unaweza kuamua kutumia stafeli nusu, tende ukapima kwenye kiganja kimoja cha mkono na maji ukaweka vikombe viwili au vitatu kutegemea uhitaji wako.

Saga vyote kwa pamoja mpaka vilainike, ikiwa unatumia blenda ya kawaida (isiyo na uwezo wa kusaga vitu vigumu) pumzisha blenda kila baada ya dakika mbili ili kuepusha kuungua au kuharibika mapema.

Hatua hiyo ikimalizika unaweza kuchuja juisi yako na ukaongeza sukari kiasi, au ukaamua kunywa bila kuchuja au kuongeza sukari kwani matunda yote tuliyotumia yana sukari.

Mpaka hapo kinywaji chako kitakuwa tayari kwa kunywa, unaweza kuongeza barafu au majani ya mnanaa kuongeza harufu na ladha.

MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

# Ipambe sehemu ya kulia chakula kwa sinki zuri

SINKI la kunawia mikono linatajwa kuwa sehemu ya pambo katika eneo la kulia chakula. Hii ni kutokana na mwonekano na muundo wake.

Mtaalamu wa mapambo ndani, Winnie Joseph, ameiambia NIPASHE katika mahojiano maalumu kwamba kumekuwa na miundo mipya ya kuvutia inayoendelea kuvumbuliwa na wana teknolojia.

Anasema katika sehemu ya chakula, imekuja miundo mipya kuanzia kwenye ramani ya ujenzi wa nyumba hadi nakshi zinazokamilisha eneo hilo.

Anasema moja ya pambo linaloongeza thamani na mwonekano wa eneo hilo ni sinki la kunawia mikono.

"Wavumbuzi wamekuja na design (muundo), mpya wa kisasa ambao unaleta uhalisia (natural), ndani ya nyumba. Sinki la kunawia la jiwe lililopolishiwa vizuri kama unavyoona," anasema Winnie akionesha baadhi ya masinki hayo.

Anasema kitu pekee kinachovutia kwenye muundo huo ni utulivu (calmness), unaoletwa na sinki hilo.

Winnie anasema masinki hayo yanapatikana kwa rangi tofauti tofauti ikiwamo nyeusi, kahawia na kijivu.

Hata hivyo, anasema muundo huo haujafuta yale ya udongo ambayo yanatumika hivi sasa kwani bado kuna watu wanaopendelea aina hiyo.

NIPASHE ambayo imetembelea maduka tofauti jijini Dar es Salaam, imebaini kuwa 'mchawi' wa aina hiyo mpya ya sinki ni bei kwani ni kubwa ikilinganishwa na ya udongo yaliyozoeleka.







# Chukua tahadhari kuepusha majanga ya moto kwenye nyumba





USALAMA wa nyumba ni jambo la msingi kuliko vyote katika maisha ya mwanadamu na ustawi wake kwa ujumla.

Mbali na vitu vingine ambavyo ni muhimu katika nyumba kuanzia maandalizi wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi, ni pamoja na kuweka mfumo mzuri wa kuepusha majanga ya moto.

Jambo hili la kutokuweka tahadhari kuhusu majanga ya moto katika nyumba, limewagharimu wengi kutokana na nyumba zao kuungua na kuteketeza mali nyingi, hivyo kumfanya mtu kurudi katika umaskini.

Peter Uvilo, mtaalamu wa kutengeneza mifumo ya umeme kwenye nyumba, anasema ziko njia mbalimbali za kutumia kukabiliana na majanga ya moto kwenye nyumba.

Mojawapo, anasema ni kuepuka kutumia vifaa duni wakati wa kutengeneza mifumo ya umeme kwenye nyumba.

Njia ya pili, anasema ni kutumia vizuri soketi na swichi za umeme pamoja na kuepuka kutumia vifaa vya umeme duni vikiwamo redio, pasi, jokofu, televisheni na jiko.

"Kutokana na ujenzi duni, si jambo la kustaajabisha kukuta nyumba moja ina soketi moja au mbili. Hili husababisha watu kujaza kila kifaa kwenye soketi hiyo moja, hivyo kusababisha soketi izidiwe na kuwaka moto.

"Njia Ya tatu, anasema ni kutumia vyema jiko lililoko ndani ya nyumba. Unatakiwa kuchukua tahadhari zaidi. Haijalishi ni jiko la umeme, gesi au mafuta. Unatakiwa kuzingatia mambo kadhaa ili kuepuka majanga ya moto. Lisafishe, usiliache likiwa na mafuta au kuacha karatasi karibu nalo," anasema.

Njia ya nne, anasema ni kuepuka kuacha moto ukiwaka karibu na nyumba bususani kwa wale wanaochoma taka.

Anashauri pia kutumia moto ulio wazi kwa uangalifu na kwamba wakati mwingine watu huwasha vibatari, mishumaa au hata sigara ndani ya nyumba nayo ni hatari.

"Ni vyema kuchukua tahadhari kabla ya janga kutokea, ni muhimu ukahakikisha nyumba yako ina miundombinu ya kukabili moto pamoja na vifaa vya kuzimia moto. Weka vifaa vya kuhisi moto au moshi.

"Hakikisha watu wanaweza kujiokoa kwa kupitia madirishani au kwenye milango ikiwa moto utatokea. Yaani jenga madirisha na milango inayoruhusu watu kujiokoa. Weka vifa vya kuzimia moto kama vile mpira wa maji wa kuzimia moto pamoja na mitungi ya hewa," anasisitiza.

Pia anashauri usitumie vitu vinavyoshika moto haraka ikiwamo mafuta ya gari, rangi, gesi, pamba. Hakikisha unachunguza kila bidhaa unayotaka kuiweka kwenye nyumba yako ili kubaini kama inashika moto haraka ili ihifadhiwe kwa tahadhari kubwa."

Lingine analoshauri ni kuchukua tahadhari umeme unapokatika kwa kuzima vifaa vya umeme.

"Tumia vifaa vya kutawala kiwango cha umeme. Hivi huhakikisha umeme unaoingia kwenye vifaa vyako ni wa kiwango kinachotakiwa na huwa na mfumo unaojulikana kama "delay" ambao hauruhusu umeme kuingia kwenye vifaa moja kwa moja mara unaporudi," anabainisha.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya***

# Utafiti waonyesha upungufu maji safi

**Na Enock Charles**

PAMOJA na jitihada za Serikali kufikisha maji katika maeneo mbalimbali wadau wameeleza bado kuna upungufu wa maji safi na salama katika maeneo mengi na kuchangia ukatili wa kijinsia vikiwamo vipigo na ubakaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania, (TGNP) Lilian Liundi, akizungumza na wadau wa maji katika ofisi za mtandao huo, mkoani Dar es Salaam juzi, aliiomba serikali kusikiliza kilio cha wananchi kuhusu suala la maji.

Wadau hao ambao ni wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa huo waliwasilisha utafiti waliofanya kuhusu suala la maji katika wilaya tatu Dar es Salaam na hali ya ukatili wa kijinsia inayotokana na ukosefu wa maji.

Utafiti wao huo ulioungwa mkono na madiwani wa Kata za Majohe na Makurumla waliofika katika mkutano huo ulionyesha kwamba, maeneo mengi yaliyofanyiwa utafiti katika Wilaya za Ubungo, Ilala na Kinondoni bado hali ya upatikanaji wa maji ni ya kusuasua, huku wengine wakisimulia visa vya ubakaji na rushwa za ngono ili kupata maji.

"Katika wilaya ya Ubungo katika watu 100 tuliowauliza kuhusu hali ya upatikanaji wa maji asilimia 21.4 walisema yanapatikana, huku asilimia 78.5 walisema hayapatikani.

"Kinondoni asilimia 57.1 walisema yanapatikana na asilimia 23.8 hayapatikani, Ilala asilimia 19.5 walisema yanapatikana na asilimia 80.5 hayapatikani," sehemu ya utafiti huo ulisema.

Madiwani hao waliahidi kutoa ushirikiano kuhakikisha maji yanapatikana na kutoa kipaumbele kwa maeneo yenye ukosefu zaidi ambayo yameainishwa katika utafiti huo.

Diwani wa Makurumla, Bakari Kimwanga, aliwapongeza wananchi kwa utafiti ambao utawasaidia kutatua matatizo yaliyoko.

"Taarifa iliyoletwa kwangu itanisaidia na nitaiwasilisha kwa Mstahiki Meya, lakini nitampa Mheshimiwa Mbunge," alisema.

Diwani wa Majohe, Paschal Linyamala, alisema atafikisha utafiti huo kwa Mbunge wa Ukonga na kuainisha baadhi ya mikakati katika kata yake ili kuwapunguzia wananchi kero hiyo ya maji ambayo alikiri bado ni tatizo katika kata yake.



Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (LAAC) wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Stansalaus Mabula, wakikagua mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Serengeti mkoani Mara wakati wa ziara ya kamati hiyo mkoani Mara. **PICHA: BUNGE**

# Raia China adakwa Dar kwa madai kuingiza vifaa kinyume cha taratibu

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watu wawili, akiwamo raia wa China, kwa tuhuma za kuingiza nchini vifaa vya mawasiliano ya mtandao wa intaneti bila kufuata utaratibu wa kisheria.

Vifaa hivyo vyenye jina la STARLINK KIT/DEVICE ambavyo vimeanza kuuzwa mtaani, vimekamatwa katika msako uliofanywa kwa kushirikiana na kikosi kazi maalum cha kuzuia na kupambana na matumizi ya makosa ya kimtandao.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema juzi jijini Dar es Salaam kuwa baadhi ya vifaa hivyo vimeshauzwa na kutumika katika baadhi ya maeneo.

Alisema kitendo hicho ni kosa na kinyume cha sheria kwa kuwa vifaa hivyo havijaidhinishwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

"Tumewakamata Claudian Makaranga (28) mkazi wa Kawe, Kinondoni na Hongliang Yang (35), raia wa China, mkazi wa Kigamboni, kwa tuhuma za kuingiza vifaa vya mawasiliano ya intanet nchini bila kufuata utaratibu wa kisheria vyenye jina la STARLINK KIT/DEVICE," alisema.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakijitangaza kuuza vifaa na kutoa huduma ya internet nchini kupitia mtandao ya kijamii wa Instagram kwa akaunti yenye jina la STARLINK.

Alisema katika msako huo vifaa vilivyokamatwa ni Starline Dish 12, Starlink Router 12.

"Tunatoa wito kwa wananchi kuwa makini na matumizi ya vifaa vya mawasiliano ambavyo havijaidhinishwa na mamlaka husika," alisema.

Wakati huo huo, Kamanda Muliro alisema wanawashikilia Wilfred Werandumi (44), mkazi wa Tungi na Abdulrahim Mwakibinga (30), mkazi wa Mwandege, kwa tuhuma za kutumia majina ya viongozi wa nchi kutapeli watu kwa kujifanya wanaomba michango ya harusi, misiba na matibabu.

"Baadhi viongozi ambao majina yao yametumika katika utapeli huu ni Dk. Stergomena Tax, Innocent Bashungwa, Mohamed Nchengerwa, Mhandisi Hamad Masauni na Katibu Mkuu wa zamani wa CCM, Daniel Chongolo,"alisema.

Kamanda Muliro alisema katika msako huo, wamewakamata Salum Kingu (25) na Loveness Silonga (24) wote wakazi wa Mbalizi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kutumia akaunti ya mtandao wa kijamii wa Facebook yenye jina la KOPA FASTER TULIA TRUST FOUNDATION na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Alisema watu hao hujipatia fedha hizo kutoka kwa watu mbalimbali kwa kudai kuwa wanatoa mikopo kwa masharti nafuu na haraka wakitumia namba ya simu 0749 704445.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na ufuatiliaji mkali wa tabia hizi na watuhumiwa wote watashughulikiwa vikali kwa mujibu wa sheria.

# Tanzania yakabiliwa uhaba wataalamu vifaa tiba

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

TANZANIA inakabiliwa na uhaba mkubwa wa wataalamu wa kutengeneza vifaa tiba vinavyoharibika, hivyo kusababisha kutupwa na kuisababishia serikali hasara kwa kununua vipya kila wakati

Kutokana na hali hiyo, serikali kupitia wadau wa elimu ya juu na mafundi sanifu wa vifaa tiba wamekusudia kuboresha mtaala wa afya katika masomo ya ufundi sanifu wa vifaa hivyo na Sh. bilioni 1.5 zimetengwa kufanikisha azma hiyo.

Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Sayansi za Afya Mvumi,(MIHS) kilichoko mkoani Dodoma, Prof. Charles Mazengo, alisema juzi kuwa kwa sasa vyuo vinavyotoa mafunzo hayo ni vitatu huku vikiendelea kukumbwa na uhaba wa walimu kutokana na kutokuwapo kozi hiyo nchini. "Tulitengeneza mtaala ambao ulikuwa lazima upitiwe na wataalamu ili watoe maoni yao kama unafaa kutumika katika kozi hizo. Kwa upande wa wataalamu wa kufundisha wanachuo, pia bado ni wachache, hivyo tunaendelea kutafuta wataalamu zaidi," alisema Prof Mazengo. Askofu Kanisa la Anglikana Tanzania, Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT), inayomiliki chuo hicho, Dk. Dickson Chilongani, alisema licha ya kozi hiyo kuanzishwa katika hospitali ya Mvumi, mkoani Dodoma katika miaka ya 1990, bado kozi hiyo haikutiliwa mkazo, hivyo bado imeendelea kuonekana ni kozi mpya kwa Tanzania.

Dk. Chilongani alisema katika uboreshaji wa mtaala huo, wadau mbalimbali walishirikishwa wakiwamo Wizara ya Afya, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTIVET) na vyuo mbalimbali ili kupitia na kusaidia uzalishaji wa wataalamu watakaotengeneza vifaa tiba katika hospitali zote nchini.

"Tumejipanga kwa kuanzisha kozi hii, kuboresha mazingira vyuoni kama vile kujenga madarasa, kununua vifaa vya kufundishia na walimu watakaofundisha na kuanza kutangaza kozi hiyo ili kupata wanafunzi wa kutosha tuondoe huu upungufu," alisema.

Mshauri kutoka Shirika la Tuimarishe Afya (HPSS), Ally Kebby, alisema mpaka sasa jitihada zimeendelea kuchukuliwa na serikali ili kupanua wigo katika eneo hilo kwa kuzalisha mafundi sanifu wa vifaa tiba wabobezi ili kuendelea kuinua sekta ya afya nchini.

Kebby akasema hadi sasa tayari mafundi sanifu takribani 250 wameshaajiriwa katika hospitali mbalimbali hapa nchini.

## HABARI KIMATAIFA




Kikosi cha uokoaji kikiendelea na kuzima moto na kutafuta waathirika baada ya shambulio la bunduki Urusi. **PICHA: AP**

# RUSSIA YATIKISWA

## -Watu 115 wauawa ukumbini
## -Islamic State yakiri kuhusika

**MOSCOW,** RUSSIA

USIKU wa kuamkia jana taifa la Russia limekabiliwa na shambulio baya baada ya watu wenye bunduki kuvamia ukumbi wa burudani na kuwaua watu zaidi ya 100 na kuwajeruhi wengine 140.

Katika tukio hilo la watu hao ambao imefahamika ni kutoka wapiganaji wa kundi la Islamic State, walifanya shambulizi hilo ndani ya ukumbi wa maonyesho ya burudani.

Kulingana na Taasisi ya Usalama ya Shirikisho la Russia, (FSB), ukumbi huo maarufu na ulioko katika eneo la Crocus katika kitongozji cha Krasnogorsk, kaskazini-magharibi mwa jiji la Moscow, unajulikana kuwa kivutio cha watu wengi kwa ajili ya kupata burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali wa kimataifa.

Baada ya tukio hilo, video ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha watu kadhaa waliokuwa na silaha wakiingia ndani ya ukumbi huo kabla ya kufyatua risasi ovyo.

Shambulio hilo lilitokea kabla ya kuanza kwa tamasha linaloitwa Picnic, ambalo bendi maarufu ya rock ilikuwa ikitaka kutumbuiza.

Awali, mamlaka ilitangaza jumla ya tiketi 6,200 za tamasha hilo zilikuwa zimeuzwa, lakini bado haijawekwa wazi watu wangapi walikuwa wameingia ndani ya ukumbi wakati shambulio hilo likitokea.

Vyombo vya habari vya Russia viliripoti kwamba washiriki wa bendi hiyo hawakuwepo wakati wa ufyatuaji risasi.

"Miili ya watu bado inaendelea kutambuliwa na mpaka jana jioni ilithibitishwa kuwa zaidi ya watu 100 walikufa katika shambulio hilo la kigaidi.

Hata hivyo, idadi ya vifo na walioathirika inaweza kuongezeka.

Wiki mbili zilizopita, ubalozi wa Marekani nchini humo ulitoa tahadhari ya usalama baada ya kupokea ripoti kwamba watu wenye itikadi kali wana mipango ya kushambulia watu kwenye mikusanyiko mikubwa jijini Moscow.

Aidha, Marekani iliwataka raia wake kuepuka mikusanyiko mikubwa ndani ya Saa 48.

**UKRAINE YAHUSISHWA**

Mkuu wa FSB, amezungumza na Rais Vladimir Putin, kuwa watu wanne waliohusika katika shambulio hilo ni miongoni mwa 11 waliozuiliwa.

Katika taarifa ya kiusalama iliyotolewa jana jioni, ilisema washambuliaji hao ambao wamekamatwa na kuweka mahabusu katika eneo la Bryansk, walikuwa na nia ya kuvuka mpaka kwenda nchini Ukraine.

Hata hivyo, Mykhailo Podolyak, ambaye ni mshauri wa Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alikanusha kuhusika kwa nchi yake katika shambulizi hilo la kigaidi.

"Haina uhusiano wowote na matukio haya". alisema

Matthew Sussex, ambaye ni mtaalamu wa masuala ya Russia katika Chuo Kikuu cha taifa cha Australia, aliambia BBC, Russia inaweza kufanya kujibu shambulio hilo.

"Urusi ina historia ndefu ya kutowatendea vema watu wengi waislamu waliopo nchini humo. Tulikuwa na vita vya aina mbili huko Chechnya, kuanzia 1999 hadi 2006 vilikuwa vita vya msimamo mkali kuna watu ambao walikwenda kupigana na Islamic State dhidi ya serikali ya Russia," alisema.

"Tangu wakati huo, shughuli za Russia nchini Syria zimewafanya Islamic State kuiona serikali ya nchi hiyo kama tishio," aliongeza.

Wakati huo huo, mataifa mbalimbali yamejitokeza kulaani tukio hilo.

Rais wa China Xi Jinping ametuma salamu kwa Rais Vladimir Putin, kulaani shambulio lililotokea ndani ya ukumbi wa Crocus.

Rais Xi alisisitiza kwamba China inapinga aina zote za ugaidi na kulaani kwa nguvu shambulio hilo na kuiunga mkono kwa nguvu zote zitakazochukuliwa na serikali ya Russia dhidi ya usalama wake wa kitaifa na utulivu.

Wakati huohuo, Waziri Mkuu wa India Narendra Modi, amelaani shambulio hilo.

Kupitia ukurasa wake wa X, Modi alilitaja shambulio hilo kuwa baya na nchi yake ilisimama kwa mshikamano na serikali pamoja na watu wa shirikisho la Russia katika kipindi cha majonzi.

**BBC**

## Russia, China zapiga kura ya turufu

**NEW YORK,** MAREKANI

NCHI za Russia na China zimepiga kura ya turufu kupinga azimio lililowasilishwa na Marekani katika Umoja wa Mataifa likitaka kusitishwa mapigano Ukanda wa Gaza.

Balozi wa Russia katika Umoja wa Mataifa, alisema rasimu hiyo ni ya kinafiki ambayo haitowi wito wa moja kwa moja wa kusitishwa kwa mapigano.

Rasimu hiyo ya azimio la Marekani, ambayo ilisisitiza juu ya haja ya usitishaji vita wa haraka na wa kudumu na kuachiliwa kwa mateka, ilipata kura 11 za ndio, kura tatu zikipinga ambazo ni za Urusi, China na Algeria na moja ya Guyana, ilijizuia kupiga kura.

Kushindwa kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kupitisha rasimu hiyo, kwa mara nyingine kumetokana na mzozo wa kidiplomasia kati ya mataifa hayo makubwa.

Kimsingi, maandishi hayo yalisisitiza "haja ya usitishaji vita wa mara moja na wa kudumu ili kulinda raia kutoka pande Marekani imezuia mara tatu maazimio ya Umoja wa Mataifa kwa kutumia haki yao ya kura ya turufu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

**RFI**




Polisi wakilinda nje ya jengo la ukumbi linalowaka moto baada ya magaidi kushambulia kwa bunduki. **PICHA: REUTERS**

## MAKALA

# KUBADILIKA KWA WATU KUMEBADILISHA MAISHA



Na Magabilo Masambu

**Kuna hoja za baadhi ya watu kutumiwa kutokana na hali zao za kimaumbile na kimaisha kutajirisha baadhi ya watu mijini. Kwamba, unamkuta mtu ni ombaomba lakini anahifadhiwa na mtu fulani na ndiye anayemtumia kuomba ili kila inapofika jioni wanagawana mapato.**

HIVI maisha yamebadilisha watu au watu wamebadilisha maisha? Dunia imebadili watu au watu wamebadili dunia? Haya ni miongoni mwa maswali ambayo kila mmoja wetu anaweza kujiuliza hasa kwa watu wenye umri mkubwa kidogo, ambao wamebahatika kuyaona na kuyaishi maisha ya nyakati zile na za sasa.

Siku moja, nikawa nasoma andiko moja la mwandishi maarufu wa mtandaoni kwa jina Malisa GJ. akieleza kisa kimoja kilichomhusisha mzee aliyekuwa maeneo ya Sinza kwa Remmy akiomba wasamaria wema wamsaidie fedha ya nauli ili arudi nyumbani kwake Kibaha na mkewe. Lakini ikaonekana watu wengi walioombwa fedha walipuuza au hawakuwa nazo au kwa sababu nyinginezo wanazozifahamu.

Kati ya watu ambao mzee huyo alikuwa amewaomba, ni mmoja tu ambaye alimpatia Sh. 1,000 tu ambayo pia haikuwa inatosha kufika Kibaha. Katika andiko lile, inaonyesha kuwa mke wa mzee huyo anaugua saratani ya ziwa na vilevile wazee hawa hawakubahatika katika maisha yao kupata mtoto, hivyo wanaishi wenyewe.

Pengine nijikite kwenye hoja ya ama kutoa msaada au kutotoa msaada kwa watu wanaoonyesha kuwa na uhitaji. Ni kweli kwamba hakuna mtu anayeweza kukidhi mahitaji yake hata akiwa na fedha kiasi gani, hivyo kuna wakati anahitaji masaada wa watu wengine. Unaweza kuwa huhitaji msaada wa kifedha, ukawa na mahitaji mengine ambayo wewe huna lakini wasio na fedha wakawa nayo.

Katika jamii zetu za Kitanzania, kwa miongo kadhaa, tumekuwa na utamaduni wa kuishi kwa kusaidiana, yaani tunaishi kijamaa. Limekuwa jambo la kawaida kuombana vitu kama vile chumvi, sukari, unga na fedha. Zamani, imani ya kusaidiana ilikuwa kubwa sana na watu waliona fahari kusaidia na waliosaidiwa walionyesha uthamani wa misaada hiyo lakini hapa katikati kumetokea sintofahamu kubwa.

Mosi, pamekuwepo na dhana za kishirikina kwamba si kila anayeomba msaada ana uhitaji. Wengine imebainika kwamba wanaomba ili wakafanye yao. Inawezekana jambo hilo lisiwe na uthibitisho wa moja kwa moja lakini mantiki na mazingira yanalazimisha watu kuamini kutokana na kuwapo kwa dhana za chuma ulete. Wako wanaoamini kwamba katika mazingira ya dunia ya leo, watu wameendelea sana katika elimu hizo zisizoonekana, kwa hiyo wanakuwa na hofu ya kusaidia kwa kuogopa kuchumwa kwa njia za giza.

Hali ya kutoamini. Tumejenga jamii isiyoaminika katika mambo mengi. Hata pale mtu anapokuwa anamaanisha kueleza jambo fulani linalomsibu, inakuwa vigumu kwa watu wanaotakiwa kusaidia kutoa msaada. Ni jambo baya sana kuwa na aina hii ya jamii lakini nani tutamlaumu kwa hili? Ni sisi wenyewe wanajamii.

Kuna hoja za baadhi ya watu kutumiwa kutokana na hali zao za kimaumbile na kimaisha kutajirisha baadhi ya watu mijini. Kwamba, unamkuta mtu ni ombaomba lakini anahifadhiwa na mtu fulani na ndiye anayemtumia kuomba ili kila inapofika jioni wanagawana mapato.

Hilo nalo limeleta ugumu katika kuamini kama kweli wanaoomba ni wao au wanapeleka fedha mahali fulani kama ambavyo tumewahi kuona katika vyombo vya habari kwenye baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam kwa baadhi ya ndugu zetu wenye mahitaji maalum, wakiwa wamehifadhiwa sehemu fulani wakitumiwa na baadhi ya watu kukusanya fedha na kuziwasilisha kila ifikapo jioni.

Sasa je, maisha yamebadili watu au watu wamebadili maisha? Katika mazingira ya namna hii, tunaweza kuwaona baadhi ya watu wanaokataa kusaidia watu wenye uhitaji kuwa wana roho mbaya, wakati sisi wenyewe ndiyo tumekuwa sababu. Tunapowalaumu kwamba hawasaidii lazima tuwe tunayakumbuka haya.

Dunia ya sasa ni vigumu sana kumwamini mtu hata kama ataonekana amevaa kanzu ya kasisi wa kanisa au imamu wa msikiti kwa sababu tunaowaamini ndio wengi wao wanaotuzamisha mashimoni. Imekuwa vigumu sana kumtambua mwenye shida ya kweli na tapeli, chuma ulete au mshirikina.

Zamani ilikuwa kawaida wenye magari kutoa lifti lakini kesi za baadhi ya watu kutekwa au wengine kukatalia kwenye magari hayo wakidai walipwe, nazo zimekuwa zikiripotiwa. Mwanamume mmoja aliwahi kumpa lifti dada mmoja na walipofika mwisho wa safari, dada akafungua vishikizo vya shati na kudai kiasi cha fedha, kama hatapewa apige kelele kwamba mwenye gari amemtumia na hataki kumlipa. Dunia sasa imekuwa duni!

Mambo haya kwa kiasi kikubwa yamewakatisha tamaa watu wema ambao wangeliweza kumsaidia yeyote. Hawawezi tena ni bora sasa waonekane wana roho mbaya badala ya kuingia matatizoni. Kwa nukta hii, naweza kukubali kwamba watu wamebadilika, hivyo lazima maisha pia yabadilike japo si wote wanaohitaji msaada. Wako wenye uhitaji tuwasaidie lakini tuwe makini.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Duniani vyote vinagawanyika, mali, shamba lakini siyo penzi*



Na Adam Fungamwango

MAPENZI na pesa ndiyo vitu vinavyosumbua watu duniani. Ni vitu ambavyo havijawahi kuzoeleka hata siku moja.

Leo hii tunazungumzia kitu kinachoitwa mapenzi. Wanasema yalianza zamani enzi za Adam na Eva, lakini hadi leo hakuna mtaalam anayeweza kusema hayajawahi kumsumbua. Hakuna tajiri wala maskini, kiongozi na raia, wote kwenye suala linaloitwa penzi ni kizungumkuti.

Siku moja nikakuta mada mtaani ikisema kama kuna mtu yeyote duniani anaweza kupenda zaidi ya mtu mmoja kwa usawa ule ule.

Mfano wako wanaume ambao wana wapenzi zaidi ya mmoja, anaweza kuwa nao wawili au watatu. Pia kuna wanaume wenye wake zaidi ya mmoja, wawili, watatu na hata wanne.

Siku hizi baadhi ya kinadada wanaweza kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja pia kwa sababu zake binafsi.

Kwenye jamii vitu hivi vipo na tunaviona, lakini je anawapenda wote kwa usawa ule ule?

Hiyo ndiyo mada ilikuwa inashambuliwa mezani.

Wapo waliosema mwanaume anaweza kuwa na mke au mpenzi zaidi ya mmoja na anawapenda wote sawa, lakini kwa mwanamke haiwezekani.

Kuna waliosema mwanaume na mwanamke wanaweza kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja na wanawapenda wote sawa. Baadhi wanapinga katakata kuwa haiwezekani.

Hakuna binadamu yoyote duniani anaweza kupenda kwa usawa.

Hata kama atapewa wapenzi 10 kukaa nao, baada ya muda fulani, atatokea tu ambaye anampenda kuliko wengine wote, na sababu huwa hazipo rasmi kwa kuwa penzi huota tu kama majani popote pale.

Waliotetea hoja hiyo wanasema ndiyo maana utaona mwanaume anaweza kufanyiwa kila kitu na mwanamke, lakini pesa zake, nguvu na akili akazihamisha kwa mtu ambaye anamsumbua kichwa tu. Kisa ni nini amempenda.

Mwanamke anaweza kutimiziwa, kujaliwa, kuenziwa na kufanyiwa kila kitu na mwanaume mpole na mcheshi, atakuwa naye kwa sababu tu ya faida ya kile anachokipata, lakini macho na mawazo yake yatakuwa kwa mwanaume mwingine, katili, mkali, asiye na chembe ya huruma.

Anampendea nini? Anakijua mwenyewe.

Waliokuwa wanatetea hoja hii, akaongeza kitu kingine kuwa kuna kupenda na kutamani.

Yoyote mwenye wapenzi zaidi ya mmoja anabebwa na kutamani, lakini linapokuja suala la mapenzi, atampenda mmoja tu kati yao. Hiyo ni kwa wanaume.

Kwa wanawake, anaweza kupenda wengi kwa sababu za kimaslahi na vingine vinavyofanana na hivyo, lakini mapenzi yataekea kwa mmoja tu. Hiyo ndiyo asili ya binadamu. Binafsi hawa nikaona hoja yao ina nguvu.

Nikaanza kukumbuka kuna wimbo mmoja wa taarabu wa zamani mwanzoni mwa miaka ya 1980, ambao ulirudiwa na Omary Sosha wenye mashairi yafuatayo.

"Itakuwaje kutupenda wawili, nawe wajua una moyo mmoja, najua utadanganya mmoja, kama yeye au mimi sijui."

Hapa maana yake kuwa anayependa wengi kuna wengine atawadanganya tu, kwa sababu ana moyo mmoja.

Anayedanganywa nani? Mara nyingi huwa ni suala la muda tu, itafahamika kwa sababu penzi siku zote haligawanyiki.

utapenda kitu kimoja tu. Vilivyobaki vyote ni tamaa na maslahi tu. Ndiyo maana hata wahenga walishasema tangu zamani kuwa vitu vyote duniani vinagawanyika, lakini penzi siku zote haligawanyiki.

Hili limeimbwa na kutolewa ufafanuzi mzuri na bendi ya Vijana Jazz, ambapo mwanzoni mwishoni mwa miaka ya 1980 walirekodi wimbo uliotungwa na Rosh Mselela, ulitwao 'Penzi Haligawanyiki.'

Mke anamlalamikia mumewe kuwa alimuomba aoke mke wa pili na atawatimizia kila kitu kwa sababu uwezo anao. Mwisho wa siku mke mkubwa analalamika kuwa penzi limezidi elemea na mke mwenzake.

"Oooh naamini eee, methali za wahenga eee, dunia hii, vyote vinagawanyika, mali na mashamba, pia vinagawanyika, aaah, aaah, siyo penzi jamani, litafanya kila njia, pande moja litazidi, aaah, aaah, siyo penzi jamani, litafanya kila njia, pande moja litazidi.

"Oooh mume wangu eee, ulinitaka radhi eee, wataka oa mke mwingine wa pili, uwezo huo wa kukutunza unao, aaah, aaah, matokeo ya penzi, limezidi elemea kwa mke mwenzangu ee, aaah, aaah, matokeo ya penzi, limezidi elemea kwa mke mwenzangu ee.

"Nakuomba sana mume wangu eee, ukumbuke japo na watoto, Nakuomba sana mume wangu yoyo, ukumbuke japo na watoto, hunijali kwa chumvi, hunijali kwa sukari, tabu nyingi ninapata na watoto, hunijali kwa chumvi, hunijali kwa sukari, tabu nyingi ninapata na watoto.

Hunijali kwa chumvi, hunijali kwa sukari, tabu nyingi ninapata na watoto, hunijali kwa mavazi, hunijali kwa malazi, kweli penzi haliwezi gawanyika eee.

"Oooh mume wangu eee, ulinitaka radhi eee, wataka oa mke mwingine wa pili, uwezo huo wa kukutunza unao, aaah, aaah, matokeo ya penzi, limezidi elemea kwa mke mwenzangu ee, aaah, aaah, matokeo ya penzi, limezidi elemea kwa mke mwenzangu ee."

Narudia na mimi kusema tena kusema hapa ulimwengwni kila kitu unaweza kukigawanya, hata dunia unaweza kuigawa katikati, lakini kwenye penzi haiwezekani.

**Tuma meseji 0716 350534**

HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AKAKUMBUKUKA alipowaambia wabomoe wenyewe nyumba ili wenye hati halisi wachukue kiwanja chao la sivyo itakuja kubomolewa kwa amri wa mahakama, au kwa kuwasaidia mawazo ni kwamba watafute wakili ili aende kortini azuie ubomoaji kwanza ili utaratibu mwingine ufuatwe.

Akakumbuka jinsi dada yake alipomwambia atafute wakili, lakini yeye akakataa na kumwambia hawezi kufanya hivyo kwa kugharamikia nyumba ambayo mkewe anateseka, hivyo ni bora aondoke wakaishi kwingine mbali na hapo ili awe na amani.

Hilo lilimfanya Havijawa kuangua kilio na kuona sasa dunia imemuelemea kwani kama kaka yake ataondoka, yeye hana uwezo wa gharama za kuweka wakili ili kuzuia nyumba kuvunjwa na kufungua kesi. Akibaki peke yake nyumba itavunjwa tu. Hivyo akaona cha kufanya ni kumlilia kaka yake afanye kama walivyoambiwa na Ofisa Ardhi ili waendelee kuishi pale wakisubiri hatma yao.

Ili kaka yake akubali hilo ni lazima mkewe awe na amani na utulivu, aishi vizuri na mkewe na amuombe msamaha, kitu ambacho Havijawa alilazimika kukubali. Hilo ndilo lililombadilisha na si kingine.

Kassim na Pembe wakati wanafanya igizo hilo walijua kabisa mwisho wake utakuwa hivyo.

"Na hata siku ya kikao cha kuomba msamaha mimi naomba nisiwe mmoja ya watakaohudhuria."

"Kwanini Pembe?"

"Kumbuka mimi nilikuja kwako na kujifanya Ofisa Ardhi, sidhani kama mtu wa aina hiyo anaweza kuhudhuria kikao cha ndugu, jamaa na marafiki. Itaanza kuzua maswali. Mimi natakiwa kuja pale na kuwaambia kuwa mambo ya kesi yenu yanakwenda vizuri, ili waendelee kuwa na amani."

Kassim alimshangaa rafiki yake Pembe kwa ushauri, mbinu na mipango aliyoitumia ambayo imefanya siku mbili tatu tu zilizopita kushuhudia mkewe na dada yake wakipika, kuongea na kula pamoja.

********************************

"Wifi, leo hii nakuomba msamaha rasmi kwa yale yote niliyokutendea huko nyuma!" Ilikuwa sauti yenye mchanganyiko wa huruma na huzuni.

"Nimekusamehe wifi yangu. Wewe ndiyo wifi yangu, sina mwingine."

Havijawa aliomba msamaha na Sauda akaukubali. Ilikuwa ni siku maalum. Iliyopangwa kwa ajili hiyo tu.

Siyo kama hawakuwa wamepatana. Tangu aliporejea kutoka Kondoa, Havijawa alimpokea wifi yake mabegi na hapo ndipo walipoanza kuongea vizuri, wakisaidia kazi mbalimbali, kupika na hata kula pamoja.




**Hili limeimbwa na kutolewa ufafanuzi mzuri na bendi ya Vijana Jazz, ambapo mwanzoni mwishoni mwa miaka ya 1980 walirekodi wimbo uliotungwa na Rosh Mselela, ulitwao 'Penzi Haligawanyiki.'**

Kila mmoja alifurahi na kila mmoja aligundua kumbe kuna kitu alikuwa akikikosa.

Wakaanza kuongozana dukani, sokoni na hata mjini kununua nguo.

Kila mmoja aliwashangaa. Mtu na wifi yake wamepatana. Watu ambao walikuwa hawaelewani kama paka na chui.

Ilikuwa wiki moja ya mabadiliko, ambapo majirani walijionea hali tofauti na ilivyozoeleka.

Ikawa sasa kila mmoja anampeleka mwenzake kwa shoga yake ili kuunganisha zaidi urafiki.

Havijawa alimpeleka wifi yake kwa shoga yake Fatuma. Hata hivyo hakujua kuwa wakati mwingine Fatuma alikuwa akikutana na Sauda kwa siri na kujadili jambo lile.

Kilichomshangaza Havijawa na kuona ni kama Sauda na Fatuma wamezoeana haraka zaidi. Hakujua walishawahi kukutana mara kadhaa, mara ya kwanza ikiwa sokoni. Na hii ni baada ya kushuhudia unyanyasaji wa Havijawa siku ile alipomfuta nyumbani ili waende kwenye Vikoba.

Sauda na Fatuma walikumbatiana na kila mmoja alikumbuka maneno waliyoongea siku ile walipokutana sokoni.

"Samahani dada kama nakufananisha!" "Wewe ndiyo mke wa Kassim ee?" "Ndiyo mimi!"

"Ooh vizuri, mimi ndiyo yule dada aliyekuja wiki ilee pale nyumbani kwenu, nilimfuata wifi yako tukaenda vikobani. Naitwa Fatuma."

"Ahaaa kweli, nimeshakutambua."

"Siku ile mwenzangu nilikuwa nimeupara mwenyewe nakwenda vikobani, leo nina kidela changu hiki cha kuendea sokoni, ndiyo maana umenisahau." Nusura Sauda acheke, lakini akajizuia.

"Enhee dada, hebu niambie wifi yangu, siku ile nilipokuja kwenu kuna hali niliikuta nikaishangaa. Mnaishi vipi na wifi yako, maana yale maneno na ule uitaji unajua sikuupenda mimi, nusu nimjibu mimi..."

"We acha tu dada yangu, makubwa, madogo yana nafuu. Nateseka dada mle ndani, mume wangu tu ndiyo ananifariji na kunisihi nivumilie."

"Pole sana wifi yangu, yaani mtu anakuja hadi kuchafua ulipopiga deki! Anakuja kurudisha uchafu wa majani uwanjani ulipofagia. Huyo si mtu mzuri. Mimi kile nilichokiona siku ile tu ilitosha kufahamu kuwa wifi yako si mtu mzuri."

Wakati wanaachiana, Fatuma akamwambia Sauda kwa sauti ndogo na dhaifu, "yameisha." Naye akajibu hivyo hivyo, "yameisha." Havijawa hakujua wana maana gani.

Sauda naye alimpeleka wifi yake kwa rafiki yake Paulina.

Siku hiyo rasmi ya kuomba msamaha wote walikuwepo. Paulina, Fatuma, na baadhi ya majirani waliokuwa mara kwa mara waanamulia na kujaribu kusuluhisha ugomvi, wakiwemo wazee wawili.

Iliandaliwa tafrija fupi. Kassim kwa furaha ya kuona sasa amani kwenye nyumba yake inatawala, dada yake na mkewe wakipatana, akaamua kuandaa karamu ndogo na kualika watu kadhaa wachache nyumbani kwake.

Mzee mmoja akawaambia washikane mikono wakiwa wamepiga magoti. Akaanza kuomba. Alipomaliza akawaambia.

"Sasa muishi kama ndugu. Atakayekiuka maagizo haya, kitakachompata atajua mwenyewe."

Agizo, au masharti hayo hayakumsumbua Havijawa kwa sababu ni kweli aliamua kubadilika.

Wakati haya yakiendelea, huko nje mapishi yaliendelea pia, na baada ya hapo watu walikula na kunywa. Kila mmoja alifurahi.

Kassim alitoka nje, na alivuta hatua nyingi kutoka nyumbani kwake hadi mtaa wa pili, akampigia rafiki yake Pembe kumwambia mambo yalivyoendelea.

"Kusema kweli nakusuhuru sana, kila kitu kimekwenda vizuri, tafrija nayo imeenda vyema na nilipenda kwenye uje, ila kama ulivyoshauri, ingeleta maswali kwa Ofisa Ardhi kuhudhiria tafrija ndogo ya kifamilia kama hii, ila tutaonana kule tunakoonana kwenye mambo yetu ya kinywaji." Alipomaliza kuongea na rafiki yake akakata simu na kurejea nyumbani ambako aliacha tafrija inafikia ukingoni.

Walibaki watu wanne tu. Havijawa na wifi yake Sauda, Fatuma na Paulina. "Havijawa unaonaje sasa tumuingize wifi yetu kwenye kikoba?"

"Aah! Kweli umenikumbusha Fatuma. Tumuingize itamsaidia sana, lakini kwa sababu atakuwa anaingia kati, kuna gharama fulani itabidi alipe. Lakini mimi nitailipa!" Akajibu Havijawa.

"Siyo wewe peke yako, na mimi pia nitatoa kiasi fulani ili kumuwezesha kuingia na mwishoni mwa mwaka tukivunja na yeye awe mtu katika watu. Lakini hebu mwenyewe atuambie labda hataki!" Fatuma alisema huku akimtazama Sauda.

"Kuna mtu hataki kuingia vikoba, tatizo marejesho tu."

"Kaka yupo bwana!" Wakati Havijawa akizungumza hayo, Kassim akaingia na kukuta mjadala ule ambao alishirikishwa kwa kifupi.

"Kama mnampeleka huko wifi yenu sina neno, mimi pesa ya marejesho ya kila wiki nitakuwa nampa mpaka akipata mwisho wa mwaka, basi atajua mwenyewe afanye biashara gani ili apate pesa ya kuwa analipa mwenyewe."

"Na mimi mnipeleke, kila kitu nitalipa mwenyewe." Paulina naye alivutiwa.

"Jamani namuomba mke wangu mara moja." Kassim alitania huku akiwa amemshika mkono.

Wote waliangua kicheko.

**MWISHO**



# LUKAMBA AKIRI VIDEO CHAFU

MSANII wa filamu na mpiga picha wa zamani wa Diamond Platnumz, Lukamba amesema hawezi kutishika na video za ngono ambazo watu wanatishia kuziachia mitandaoni.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Lukamba amesema anajua sehemu alizopata mtu anayetishia kuziweka mtandaoni .

Amekiri mwanaume ambaye alionyeshwa kwenye video hiyo ni yeye na kwamba ilikuwa zamani wakati akiwa ndani ya nyumba ambayo alikuwa akiishi na mpenzi wake wa zamani.

"Napigiwa simu sana na kutumiwa screenshot zikinionesha nipo chumbani hapo ni nyumbani tulipo kuwa tunaishi mimi na mpenzi wangu na hizo vipande au video anazo huyo mpenzi wangu ni za muda," amesema Lukamba.

Hata hivyo kuachana katika mapenzi sio vita na amevumilia mengi baada ya kuongelewa maneno ya uongo kuhusu yeye na sasa watu hao wamekuja na njia nyingine ambayo wanamtafuta.

# *Masunga Masala awang'ata sikio vijana*

MWIMBAJI anayekuja kwa kasi kwenye muziki wa Injili nchini, Masunga Masala, amewashauri vijana kumtumikia Mungu wakiwa na nguvu.

Akizungumza na Nipashe, Masunga amesema wimbo wake wa 'Tumika kwa Bwana' unawakumbusha watu kuwa wameumbwa kutokana na kusudi la Mungu ili wamjue, wampende na wamtumikie.

"Lengo la wimbo wangu ni kuwakumbusha vijana waone wana deni katika kumtumikia Mungu wakiwa na nguvu sio mpaka wazeeke au wachoke,uwe mchungaji, mwinjilisti au mwimbaj unaweza kutumika kwa mali au fedha au kutoa muda wa kufanya usafi kwenye nyumba za ibada," amesema Masunga.

Aidha Masunga alimshukuru Mchungaji Kiongozi wa kanisa la FLJS, Nickson Mafuru kwa kuwapa nafasi vijana ya kumtumikia Mungu akiwamo yeye ambaye ameanza kupata mafanikio.



## ZISIKUPITE

### ALEXANDER-ARNOLD ALENGWA

REAL Madrid imeongeza shauku ya kumnunua beki wa kulia wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold, 25, huku mkataba wa mchezaji huyo huko Anfield ukitarajiwa kukamilika mwaka ujao. ***(Relevo)***

### ALOSO KUTUA BAYERN

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso atajiunga na Bayern Munich badala ya Liverpool ikiwa atahamua kuondoka kwenye klabu yake ya sasa msimu huu wa joto. ***(Sky Sports News)***

### BOMPASTOR ATAJWA CHELSEA

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo ya juu na Lyon kuhusu kumteua Sonia Bompastor, kiungo wa kati wa zamani wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 43, kuchukua mikoba ya Emma Hayes katika timu ya Wanawake. ***(ESPN)***

### ENDRICK AWANIWA CHELSEA

CHELSEA inaongoza mbio za kumnasa mshambuliaji wa Brazil, Endrick, 17, lakini wasiwasi ni ada kubwa ya kumsajili kinda huyo anayekipiga Real Madrid akitokea Palmeiras. ***(Telegraph)***

### BREMER ATAKIWA MAN UTD

MANCHESTER United ipo tayari kumnunua mlinzi wa Brazil, Gleison Bremer, 27, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 43 katika mkataba wake na Juventus. ***(Mirror)***

### RAMSEY KUPIGWA BEI

KLABU ya Aston Villa huenda ikalazimika kumuuza kiungo wa kati wa England, Jacob Ramsey, 22, ili kusaidia kuepuka kukiuka sheria za faida na uendelevu. ***(Football Insider)***

### ISAK KUPIGWA BEI

KLABU ya Newcastle United huenda ikalazimika kumuuza mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak, 24, msimu wa joto ili kuzingatia kanuni za haki sawa za kifedha. ***(Football Insider)***

### CLARKE BASI TENA

WINGA wa Sunderland, Jack Clarke, 23, hatatia saini mkataba mpya katika klabu hiyo ya Championship ambayo inaweza kuibua shauku mpya kwa muingereza huyo kutoka West Ham na Lazio. ***(I)***

### KUREJEA DORTMUND

ALIYEKUWA mkuu wa uajiri wa Arsenal, Sven Mislintat anaweza kurejea Borussia Dortmund kama mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo. ***(Sky Sports German)***

### GREENWOOD HAKIELEWEKI

MATUMAINI ya klabu ya Getafe ya kumsajili tena kwa mkopo mshambuliaji wa England, Mason Greenwood, 22, msimu ujao yanatazamiwa kukatizwa huku Manchester United wakihitaji mkataba wa kudumu iwapo wataamua kumwacha. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE: MNAMKOSEA HESHIMA TEN HAG

**LONDON,** England

### Amesema uvumi wa kumuhusisha na kazi ya kuinoa Manchester United si sawa...

KOCHA wa England, Gareth Southgate amesema uvumi unaomhusisha na kibarua cha kuinoa Manchester United kuwa ni "ni kumkosea heshima kabisa" bosi wa sasa Erik ten Hag na kusisitiza kuwa hatazungumza na upande wowote unaoonesha kuvutiwa nae hadi baada ya Euro 2024.

**Southgate mwenye umri wa miaka 53 amekuwa kocha wa 'Simba Watatu' hao tangu 2016, lakini mkataba wake wa sasa unamalizika Desemba na alifichua kwamba alifikiria kuondoka baada ya England kufungwa na Ufaransa kwenye robo fainali ya Kombe la Dunia 2022.**

ESPN iliripoti mapema mwezi huu kwamba Southgate anatazamwa kama mgombea anayewezekana kuchukua nafasi ya Ten Hag huku wamiliki wapya, Ineos wakiendelea na juhudi zao za kubadilisha nyadhifa kuu za United.

Akizungumza kabla ya mechi ya kirafiki ya England dhidi ya Brazil jana kwenye Uwanja wa Wembley, Southgate alisema: "Nadhani kuna mambo mawili kwa mtazamo wangu, moja ni kwamba mimi ni kocha wa England, nina kazi moja kimsingi najaribu kutwaa ubingwa wa Ulaya. Ni wazi kabla ya hapo, kuna michezo miwili muhimu wiki hii.

"Jambo la pili ni kwamba, Manchester United ina kocha na nadhani siku zote ni kukosa heshima kunapokuwa kocha sehemu unayohusishwa nayo. Mimi ni rais wa (Chama cha Makocha wa Ligi), hivyo sina muda wa aina hiyo."

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba chama cha soka cha England, FA, kinatamani Southgate kubakia hadi Kombe la Dunia la 2026, lakini amesema hatafanya uamuzi juu ya mustakabali wake hadi baada ya fainali za euro msimu huu wa joto.

Akishinikizwa kujua kama bado ndivyo hivyo, Southgate alisema: "Nadhani nimejibu hili kila mara nilipokaa nanyi. Mtazamo wangu ni Ubingwa wa Ulaya. Kama tungefanya mkataba hapa awali basi kila mtu angekuwa akisema, ' Kwa nini unatia saini mkataba kabla ya Euro ambapo unapaswa kujithibitisha?'

"Kwa hakika sitazungumza na mtu mwingine yeyote na wala sijawahi. Nimekuwa katika kazi hii kwa miaka nane na siwezi kuburudisha nikizungumza na mtu mwingine wakati niko kazini, kwa hiyo sijui kama nitajibu swali lako," alisema Southgate

HABARI MICHEZO

# MBAPPE BADO ATAKA KUCHEZA OLIMPIKI




**PARIS,** Ufaransa

HUKU kukiwa na majadiliano juu ya kuhamia Real Madrid, fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe amesema kwamba bado ana matumaini ya kushiriki michezo ya Olimpiki ya Paris msimu huu wa joto na kwamba hakuna mtu ambaye bado amemwambia hataweza kushiriki.

Mbappe anatarajiwa kujiunga na Madrid wakati mkataba wake na PSG utakapomalizika msimu huu wa joto, huku ESPN ikiripoti mwezi uliopita kuwa miamba hao wa LaLiga wana matumaini ya kukamilisha makubaliano na mchezaji huyo hivi karibuni.

ESPN imegundua kuwa Real Madrid ilituma barua pepe kwa Shirikisho la Soka la Ufaransa mapema mwezi huu ikieleza kwamba haitamwachia mchezaji wao yeyote ili ashiriki kwenye michezo ya Olimpiki.

"Siku zote nilikuwa na nia sawa. Nimekuwa nikisema kwamba nilitaka kwenda kwenye Olimpiki, lakini hainitegemei mimi," alisema Mbappe katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mechi ya kirafiki ya Ufaransa dhidi ya Ujerumani jana Jumamosi.

"Siwezi kusema chochote kwa sababu hakuna aliyeniambia chochote. Ikiwa siwezi kushiriki Olimpiki iwe hivyo. Ninaposema hakuna mtu aliyeniambia chochote, nazungumzia PSG. Nina mkataba na PSG na hawajasema lolote kuhusu Olimpiki. Hatujaijadili," aliongeza.

Nahodha huyo wa Ufaransa alikataa kuzungumzia mustakabali wake kwa klabu hiyo, lakini akasema anatarajia suluhu kabla ya majira ya joto.

"Bado sijatangaza chochote kwa sababu sina cha kutangaza ... nasikitika sina cha kukuambia," alisema, kabla ya kuongeza baadaye: "Nadhani yote yatatatuliwa kabla ya Euro."

Mchezaji huyo wa PSG hakuwahi kuitaja Real Madrid wakati wa mkutano na waandishi wa habari, lakini mazungumzo kati ya kambi ya Mbappé na viongozi hao wa LaLiga yanaendelea, chanzo kiliiambia ESPN.

# Real Madrid wajitosa kwa Alexander-Arnold

**MADRID,** Hispania


MLINZI wa kulia wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold yuko kwenye rada za Real Madrid kabla ya kumalizika kwa mkataba wake mwaka 2025, kwa mujibu wa ripoti.

Alexander-Arnold yuko katika miezi 18 ya mwisho ya mkataba wake wa sasa na bado hakujawa na mazungumzo ya kuongeza muda, na Liverpool kwa sasa wanafanya kazi ya kutafuta kocha mpya baada ya kufikia makubaliano ya kumwajiri Richard Hughes kama mkurugenzi wao mpya wa michezo.

Hali mbaya ya mkataba wake imeibua nia ya Madrid ambao, kama ilivyooneshwa kwa mara ya kwanza na gazeti la Relevo likisema, "wanafuatilia kwa kina mustakabali wa Alexander-Arnold kule Anfield."

Madrid wanawinda suluhu ya muda mrefu katika nafasi ya beki wa kulia, huku nyota wa sasa Dani Carvajal alifikisha miaka 32 Januari mwaka jana, na timu hiyo ya Hispania inafahamu kuwa inakaribia wakati muafaka kumnunua Alexander-Arnold.

Kuhimiza malengo ya kukataa nyongeza imekuwa mkakati muhimu kwa Madrid katika miaka ya hivi karibuni.




# Conte kumfuata Kane Bayern Munich



**MUNICH,** Ujerumani

MIAMBA ya soka ya Ujerumani Bayern Munich imeripotiwa kuwa na mpango wa kumchagua Antonio Conte kuwa kocha wao mpya, imeelezwa.

Kocha huyo kutoka nchini Italia amekuwa hana kazi tangu Machi mwaka jana alipofutwa kazi kule Tottenham Hotspur.

Lakini, anaweza kushawishika na nafasi hiyo ya kwenda kufanya kazi Ujerumani kwa mara ya kwanza kutokana na Bayern Munich kudaiwa kuhitaji huduma yake.

Na hilo litampa nafasi ya kwenda kufanya kazi na mshambuliaji, Harry Kane kwa mara nyingine baada ya awali kuwa pamoja kwenye kikosi cha Tottenham.

Conte anatazamwa na Bayern kama mtu muhinu kwenda kuchukua mikoba ya kocha Thomas Tuchel, ambaye ataachana na miamba hiyo ya Allianz Arena mwishoni mwa msimu huu 2023/24.

Hata hivyo, tatizo linaweza kuwa kwenye kufikia makubaliano, ambapo Conte atahitaji mshahara mkubwa baada ya kuvuna pauni milioni 15 kwa mwaka alipokuwa Spurs.

Bayern ina majina ya makocha kadhaa inayowafikiria kuwapa kazi, akiwamo wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso.

Conte mwenye umri wa miaka 54, alishinda taji la Ligi Kuu England na Ligi Kuu Italia, Serie A.

HABARI MICHEZO

## Kocha mpya aichambua Tabora Utd

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Tabora United, Denis Goavec ameanza kazi rasmi kukinoa kikosi hicho lakini ameweka wazi mapungufu ya timu hiyo akianzia na safu ya ushambuliaji baada ya kufuatilia mikanda ya video ya baadhi ya mechi.

Aidha, kocha huyo raia wa Ufaransa aliendа mbali na kusema tatizo lingine la timu yake ni namna ya kuunganisha timu na kutengeneza nafasi za kufunga.

Goavec amepea jukumu la kukinoa kikosi cha tabora United baada uongozi wa timu hiyo kuvunja mkataba na aliyekuwa kocha wao Mserbia, Goran Copunovic, ambaye hakuwa na wakati mzuri kwenye timu hiyo.

“Mimi ni mtu wa kutaka kupambana, nafanya kazi kwa malengo, ninachohitaji tuungane mimi, viongozi, wachezaji na mashabiki ili tuwe kitu kimoja kwa ajili ya kusaka ushindi.

“Nimengalia baadhi ya michezo na vipo vitu ambavyo nimevigundua tunahitaji kuvifanyia kazi, kwanza nimegundua safu ya ushambuliaji ina shida, timu inatengeneza nafasi chache na inafunga mabao machache, kwa hivyo lazima kwanza tuanze na yale mapungufu makubwa ambayo nimeyagundua,” alisema kocha huyo.

Aidha, alisema atayafanyia kazi mapungufu yote na kujenga kikosi chenye uwiano sawa na anaamini kitafanya vizuri kwenye michezo iliyobaki mbele yao.

Aidha, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Thabit Kandoro amesema wamefurahi sana kupata kocha huyo akisema anaamini sasa kile ambacho wamekiwekeza kitaonekana uwanjani.

Alisema kwa muda mfupi tu wa kumtazama amegundua kuwa ni mtu ambaye anajua vitu vingi na mfuatiaji sana wa mambo na hiyo inatia moyo kuwa na kocha ambaye anaanza kazi na timu huku akiwa anajua mapungufu.

“Sisi tuna wachezaji 11 kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika, wametoka katika klabu kubwa kwa hiyo uwekezaji huu ni lazima uonekane uwanjani kitu ambacho tulikuwa hatukioni, baada ya kuongea na kocha huyu kuna baadhi ya vitu ambavyo ametuambia, tumeona ni kweli anaweza akavifanya, nimeona siku ya kwanza tu amewaita mchezaji mmoja mmoja na nimefarijika kufahamu mipango yake,” alisema Kandoro.

Tabora United inashika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 21, ikisalia na michezo tisa tu kuhitimisha msimu.

# MOROCCO AFURAHIA UPAMBANAJI TAIFA STARS

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupoteza mchezo wa juzi dhidi ya Bulagaria kwa kubali kipigo cha bao 1-0, Kaimu Kocha Mkuu wa timu ya taifa ‘Taifa Stars’, Hemed Suleiman ‘Morocco’ amesema amefurahishwa na hali ya upambanaji iliyoonyeshwa na wachezaji na ana matumaini ya kupata ushindi kwenye mchezo wao wa leo katika michuano hiyo maalum ya FIFA ‘FIFA Series 2024’.

Taifs Stars leo inashuka tena kwenye uwanja wa Dalga katika mji wa Baku nchini Azerbaijan kuumana na Mongolia.

Akizungumza na Nipashe jana, Morocco alisema kitu cha faraja kwake ni kuona kuna hali ya upambanaji imeongezeka ndani ya kikosi na kama benchi la ufundi watajitahidi kukazia hapo ili kufanya wachezaji waimarike zaidi.

**Alisema sio rahisi kwa hali ya hewa waliyokutana nayo nchini humo wachezaji kuwa na muendelezo mzuri kwa dakika zote 90.**

“Tumeona mapungufu tunayafanyia kazi, tutaweza kufanya vizuri zaidi kama tukipata muda, lakini hata hali ya hewa imekuwa chanzo cha kupoteza mchezo, kwa kuwa tulipata nafasi ya kujaribu kuisukuma timu mbele ilikuwa inaonekana kuna kitu tungeweza kufanya kama tungekuwa makini kidogo,” alisema Morocco.

Aliongeza kuwa vijana wake waliweza kumiliki mpira kama ilivyo falsafa yake na anaamini kama wataendelea kufanya hivyo na kutengeneza nafasi nyingi wanaweza kufanya vizuri kwenye mchezo wa leo.

“Tunahitaji kufanya mazoezi zaidi ili tuweze kupata muendelezo wa kiwango hiki kwa muda mwingi wa kumiliki mpira, wachezaji wote wanalingana lakini tunahitaji kuongeza hali ya kupambana zaidi, tumeona makosa yetu kwenye mchezo wa jana (juzi), naamini kwenye mchezo ujao (leo) tutafanya vizuri zaidi,” alisema kocha huyo.

Kwa upande wake, nahodha wa kikosi hicho kilichopo kwenye michuano hiyo, Himid Mao alisema mpira ni mchezo wa nafasi hivyo inapopatikana nafasi ni lazima waitumie na kuendelea kujifunza.

“Mechi ilikuwa imegawanyika asilimia 50 kwa 50 wao walikuwa na nafasi na sisi tulikuwa na nafasi, katika nafasi walizopata moja wakaitumia ila matokeo yalikuwa sawa kabisa, kama wachezaji na benchi zima la ufundi wameona nini kilikosekana pale tutaenda kwenye uwanja wa mazoezi kurekebisha kwa ajili ya michezo inayokuja,” alisema Himid.



Wachezaji wa timu ya Kitunda FC, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Wachezaji Yanga wasaka nguvu ‘Gym’*

INATOKA UK. 24

son alisema wapo kwenye maandalizi makali kwa sababu ni mechi ambayo itakwenda kuamua hatma ya klabu yao kwenye michuano ya kimataifa msimu huu.

Walter amewata wanachama na mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi katika mechi hiyo.

“Hili jambo tusiwaachie wachezaji tu peke yao, mashabiki nao wanatakiwa wawe sehemu ya historia ya mechi hii kubwa, tunawahimiza waje kwa wingi uwanjani kuwapa nguvu wachezaji,” alisema Walter.

Yanga inatafuta kuweka rekodi mpya ya kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kukaa miaka 25 bila kufika hata hatua ya makundi ya michuano hiyo mikubwa zaidi Afrika kwa ngazi ya vilabu.

## *Benchikha awapa wachezaji mapumziko*

INATOKA UK. 24

mwisho tulionyeshana ushindani na ninaamini wachezaji wanapotuliza akili na kupambana zaidi kwa kufuata maelekezo watafanikiwa kupata matokeo mazuri ya ushindi,” alisema Benchikha.

Aliongeza kuwa amekuwa akifanya kikao na wachezaji wake na kuwaeleza mipango na umuhimu wa mchezo huo ambapo baadhi ya nyota wa timu hiyo ni mara yao ya kwanza kucheza hatua hiyo.

Katika hatua nyingine, kiungo Mshambuliaji wa timu hiyo, Willy Essomba Onana, alisema huu ni wakati muhimu kwa timu yake kwenda kuandika historia mpya barani Afrika kwa kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya kwanza.

Alisema anajua wanaenda kupambana na bingwa mtetezi hivyo hautakuwa mchezo rahisi kwao lakini ndio wakati wa kwenda kuonyesha ubora wao kwa kutimiza malengo yao ya muda mrefu.

“Binafsi najisikia vizuri kucheza robo fainali kwa mara ya kwanza, Al Ahly ni kama Real Madrid kwa Afrika inaweza kuwa kwenye kipindi cha mpito lakini kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wanakuja kivingine.

“Hivyo tunajua tunaenda kucheza na timu kubwa sana Afrika hizi ni nyakati bora kwa wachezaji na viongozi wa benchi la ufundi kuandika historia mpya,” alisema Onana.

Alisema alikuwa akiingalia Simba ikiishia hatua ya robo fainali lakini ni wakati wa kwenda kubadili historia.

# Michezo

Jumapili Machi 24, 2024

Nipashe




'Mnamkosea heshima ten Hag' UKURASA 21

# Wachezaji Yanga wasaka nguvu 'Gym'

## Kocha Gamondi awaandalia dozi Mamelodi, awataka wachezaji...

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebaki siku tano kabla ya mchezo wao wa kwanza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wachezaji wa Yanga wameanza mazoezi maalum ya 'Gym' kwa ajili ya kuongeza nguvu ya miili yao.

**Wachezaji hao wa Yanga wamepangiwa muda maalum wa kufanya mazoezi hayo chini ya kocha wao wa viungo Mmorocco Taibi Lagrounihuku pia wakiendelea na mazoezi ya uwanjani.**

Kocha wa timu hiyo, Miguel Gamondi akizungumza na Nipashe jana, alisema mazoezi hayo ni moja ya programu maalum kuelekea kwenye mchezo huo muhimu.

"Kuna vitu nataka kuviongeza kwa wachezaji, mchezo unaofuata ni mchezo muhimu sana, ni lazima kujipanga vizuri na kuhakikisha tunakuwa kamili kwa asilimia zote, mazoezi ya gym yatawaongezea nguvu wachezaji lakini pia tunafanya mazoezi ya kutafuta kasi," alisema Gamondi.

Alisema wanaendelea na mazoezi yao bila kusikiliza maneno ya watu au kuangalia nini mpinzani wao anafanya.


"Maandalizi yanaendelea, kwa sasa hakuna muda wa maneno, ni kujiandaa tu na mechi, kimbinu na kiufundi, nataka wachezaji wangu waelekeze akili zao kwenye mchezo wetu ujao," alisema kocha huyo.

Aidha, alisema yeye (Gamondi) na wenzake kwenye benchi la ufundi tayari wameandaa mbinu za kuimaliza Mamelodi Sundowns kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa.

"Tuna michezo miwili dhidi yao, kila mchezo utakuwa na mbinu zake, akili yetu kwanza ipo kwenye mchezo huu wa nyumbani baada ya hapo tutajipanga kwa mchezo wa marudiano ugenini," alisema Gamondi.

Wakati huo huo, Meneja wa timu hiyo, Walter Harri-

INAENDELEA UK. 23



Gamondi

# Kocha Benchikha awapa wachezaji wake mapumziko maalum kambini Zanzibar



**Na Saada Akida**

WAKATI wakiendelea kujifua kuelekea kwenye mchezo wao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wachezaji wa Simba wametengewa muda maalum wa mapumziko.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka Zanzibar walipoweka kambi, Kocha wa timu hiyo, Abdelhak Benchikha amesema licha ya mchezo mgumu walionao wiki ijayo amewataka wachezaji wake kuwa na muda wa kupumzisha akili zao na kujielekeza sana kwenye mchezo huo dhidi ya Al Ahly.

Benchikha, alisema mechi dhidi ya Al Ahly ni mchezo muhimu na wanatambua ubora wa Al Ahly, lakini wachezaji wake hawatakiwi kuhofia zaidi ya kujiweka na kuufikiria mchezo huo na jinsi ya kwenda kupambana na kutafuta ushindi siku hiyo ya Ijumaa.

Alisema licha ya kufanya mazoezi mara mbili kwa siku lakini ametenga muda maalum kwa ajili ya wachezaji wake kupumzisha akili zao ziwaze mchezo huo tu.

Alisema kulingana na programu zake kuelekea mchezo huo, kambi ya Zanzibar inawasaidia hasa wachezaji wake kulingana na mazingira ya kufanyia kazi na kuwataka kusahau yote na kutambua umuhimu wa mchezo dhidi ya Al Ahly.

"Tunahitaji kufanya mazoezi mara mbili kwa siku asubuhi na usiku, lakini pia wachezaji kupata muda wa kupumzisha akili yao kujielekeza zaidi katika mchezo wetu muhimu.

"Tunafahamu ubora wa Al Ahly na tumecheza nao mara kadhaa na mara ya

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >